





**Mchungaji** KKKT adai kutishiwa maisha na waumini

UKURASA 16





# Nipashe

Ijumaa Aprili 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580909

www.ippmedia.com

digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




# Bunge lataja aliko Ndugai

UKURASA 2



Rais, Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais mstaafu wa Zanzibar, Alhaj Dk. Amani Abeid Karume, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo na Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, wakiitikia dua ya kumwombea Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, ikisomwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi (kulia) kwenye kaburi lake, katika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia, Mwinyi waongoza dua ya kumwombea Karume

UKURASA 3



## Mbunge aibua hoja kupanda mishahara

• **Ni** kutokana na mfumuko wa bei, Naibu Spika ampongeza... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **YANGA: BADO WAO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (kulia), akiwasha mshumaa wakati wa kumbukumbu ya miaka 28 ya mauaji ya Kimbali nchini Rwanda mwaka 1994, iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Balozi wa Rwanda hapa nchini, Meja Jenerali Charles Kalamba. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge aibua hoja kupanda mishahara

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Vwawa, Japhet Hasunga (CCM), amesema kuna haja ya kutoa motisha kwa watumishi wa umma kwa kupandisha mishahara yao ambayo haijapandishwa kwa miaka sita sasa kutokana na serikali kutokuwa na uwezo kifedha.

Vilevile, amesema kuwa sasa ni muda mwafaka kuhakikisha hatua kama hiyo inachukuliwa kwa wenzao wa sekta binafsi ili kukabiliana na mfumuko wa bei uliopo.

Hasunga, mtaalamu wa ukaguzi wa hesabu za fedha mwenye kiwango cha CPA katika uhasibu, aliwasilisha hoja hizo bungeni jijini hapa juzi alipochangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha.

"Serikali iangalie namna ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma katika bajeti hii inayofuata. Yakiboreka, hao pia watatoa ajira kwa Watanzania wengine kwa sababu watawekeza kwenye miradi na kuajiri vijana.

"Tunapoangalia maslahi ya watumishi wa umma, tuangalie na sekta binafsi. Kwa sasa ni takribani miaka 10 vima vya chini vya mishahara havijawahi kurekebishwa kisheria toka wakati huo licha ya kuwapo kwa mfumuko wa bei.

"Fedha wanazolipwa watumishi katika sekta binafsi ni kidogo sana, haziwawezeshi kuchangia Pato la Taifa vizuri, ni vizuri serikali sasa ikaangalie wafanyakazi wa sekta binafsi na hata vima vya chini vya sekta binafsi, iwe ni kwenye kilimo, uvuvi, iwe kwenye maeneo gani, maeneo yote ya sekta binafsi, zipo zaidi ya sekta 12 ambazo tulipanga vima vya chini.

"Kuna maeneo tulisema kima cha chini ni Sh. 100,000 hadi 150,000. Tangu mwaka 2013 mpaka leo wanalipa Sh. 100,000, ni nani anayeweza kuishi kwa kiwango hicho cha fedha?" Alihoji.

Pia, aliishauri serikali kuandaa mdahalo wa kitaifa ili kupata 'dawa' ya kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana nchini.

Alisema hotuba ya Waziri Mkuu imegusa maeneo yote yaliyofanyiwa kazi na serikali katika kipindi cha mwaka mmoja, akisema kama serikali ikiendelea kufanya hivyo katika miaka minne ijayo, kutakuwa na mafanikio makubwa nchini.

Hasunga pia alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio hayo, hasa kwa kuifungua nchi kiuchumi na kuimarisha demokrasia nchini.

HOJA NYETI

Alisema kuna mambo makubwa yanatakiwa kufanyiwa kazi na serikali ili kuleta maendeleo ya nchi, mojawapo ikiwa ni tatizo la uhaba wa ajira kwa vijana.

Alisisitiza vijana wengi nchini wanahitimu vyuo vikuu na vya kati, lakini wengi wao fursa za ajira wanaambulia patupu, akionya kuwa hali hiyo isipochukuliwa hatua kwa kuja na mikakati ya kuitatua, itakuwa bomu kwa nchi.

"Kwa hiyo, ninafikiri hiki ni kipindi pekee ambacho lazima tuangalie suala la ajira, na suala la ajira haliwezi kushughulikiwa na serikali peke yake, linahitaji sekta binafsi iliyo strong (imara) ambayo ndiyo itachukua vijana wengi waliohitimu katika vyuo vyetu.

"Tunahitaji kuwa na viwanda vingi na sekta mbalimbali zifanye vizuri ili ziajiri hawa vijana wengi ambao wamesoma taaluma mbalimbali. Ninaipongeza serikali imeshasema 'tutatoa ajira zaidi ya 32,000 hivi karibuni', ninaipongeza sana serikali kwa hatua hizo, hongereni sana!

"Lakini hiyo itakuwa ni hatua moja, bado tunahitaji ajira nyingi zaidi. Vijana wanaohitimu ni takriban 90,000 mpaka laki moja (100,000) kwa mwaka. Kwa hiyo, hiyo (32,000) haitoshi.

"Sehemu ambayo wanakwenda kuajiri zaidi ni kwenye ualimu na afya, lakini zipo sehemu zingine, zipo taasisi zingine ambazo tunahitaji wawe na ajira kwa sababu kuna tatizo la uhaba wa watumishi -- kuna wahasibu, kuna wagavi, kuna wahandisi, kuna maofisa utumishi na maeneo mengine yenye tatizo hili.

"Kwa namna ambavyo Waziri Mkuu ameratibu mambo mbalimbali, ninashauri hata kwenye hili la ajira kuwe na mdahalo wa kitaifa wa kuzungumzia namna ya kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu ili Watanzania wote tushirikiane, tuangalie kwa undani tufanye nini ili kutoa ajira kwa vija wetu," alisema.

FURSA DRC

Katika hoja yake ya tatu, Hasunga alitaka serikali kuanzisha bandari kavu Tunduma kwa kuwa nchi nyingi kwa sasa zinajiandaa kufanya biashara na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya nchi hiyo kujiunga kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Ni vyema sasa tukajiandaa kufungua bandari kavu pale Tunduma, tukifungua pale itasaidia wale Wakongo, Zambia na nchi zingine kusafirisha mizigo yake na TAZARA, tutafanya vizuri sana na uchumi wetu utaimarika

"Sambamba na hilo, serikali iimarishe reli yetu ya TAZARA maana kwa Mheshimiwa Naibu Spika (Mussa Zungu) TAZARA inafanya vibaya, inafanya vibaya kwa sababu hatujaipa uzito inaostahili.

"Hili shirika tangu limeanzishwa ni la nchi mbili, inawezekana upande wa pili wasione manufaa kuiimarisha hii TAZARA lakini kwa nchi kama ya kwetu ambayo uzalishaji mkubwa uko kwenye nyanda za juu kusini, tunapaswa kuiimarisha reli hii," Hasunga alihitimisha huku Naibu Spika Zungu akimpongeza kwa kuwasilisha mchango mzuri bungeni.

Wabunge wengine waliochangia mjadala huo ni pamoja na wa Mtoni, Zanzibar, Abdulhafar Idrissa, aliyeitaka serikali iiunde tume ya kushughukia magonjwa yasiyoambukiza, kama ilivyofanywa kwa baadhi ya magonjwa.

Mbunge wa Ngara, aliipongeza serikali kwa kufuta tozo 42 kati ya 47 zilizokuwa zinalalamikiwa kwenye zao la kahawa na kutangaza kutoa ajira mpya 32,000 kwa sekta za elimu na afya.

# Bunge lataja aliko Ndugai

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

UONGOZI wa Bunge umetaja aliko aliyekuwa Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa mkoani Dodoma, Job Ndugai.

Ndugai hajaonekana katika shughuli rasmi za chombo hicho tangu taarifa za kujiuzulu kwake wadhifa huo zilipotangazwa Januari 6, mwaka huu kwamba aliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na nakala kuwasilishwa kwa Katibu wa Bunge kutoa taarifa juu ya uamuzi wa kuachia ngazi.

Mara ya mwisho Ndugai kuvaa joho la Spika na kuongoza kikao cha Bunge ilikuwa Novemba 12, mwaka jana, siku ambayo pia ulikuwa ukomo wa Mkutano wa Tano wa Bunge la 12.

Hii ina maana kwamba Ndugai hakuhudhuria vikao vyote vya Mkutano wa Sita wa Bunge la 12 vilivyofanyika kwa wiki tatu Februari mwaka huu na sasa bado hajaanza kushiriki vikao vya Mkutano wa Bunge la Bajeti vilivyoanza Jumanne ya wiki hii, vikitanguliwa na shughuli za kamati za kudumu za Bunge.

Alipotafutwa na Nipashe jana kwa simu kuzungumzia kutoonekana huko bungeni kwa Mbunge wa Kongwa, Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, alisema Ndugai yuko jimboni kwake.

"Ninachokijua mimi (Ndugai) yuko kwa wananchi jimboni kwake. Hayupo bungeni maana yake yuko jimboni," kiongozi huyo wa Bunge alisema.

Nipashe ilipotaka kupata ufafanuzi kama Ofisi ya Katibu wa Bunge ina barua ya kutoka kwa Ndugai ya kuupa taarifa uongozi wa chombo hicho kuhusu kutohudhuria kwake bungeni, Katibu wa Bunge alisema:

"Sina barua kuhusu suala hilo. Mbunge asipokuwapo bungeni, maana yake yuko jimboni kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge."

Nipashe ilipohitaji ufafanuzi wa uongozi wa Bunge kuhusu wananchi wa Jimbo la Kongwa kukosa uwakilishi bungeni na mustakabali wake, Katibu wa Bunge alisema:

"Ni mapema mno, ndiyo kwanza kumefanyika vikao viwili vya Mkutano wa Bunge la Bajeti, tulianza Jumanne... (Ndugai) ana muda wa kutosha, atakuja kuungana na wabunge wenzake kushiriki vikao vya Bunge."

Kanuni za Kudumu za Bunge zinaelekeza kuwa miongoni mwa sababu za kukoma kwa hadhi ya ubunge ni kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Bunge pasina kutoa taarifa kwa Spika.

Sababu zingine ni pamoja na kifo, kufutwa uanachama wa chama cha siasa, kujiuzulu ubunge na kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai yanayosababisha kifungo cha zaidi ya miezi sita gerezani.

Nipashe ilipomtafuta Ndugai kwa simu jana saa 6:48 mchana, simu yake ya kiganjani iliita kwa sekunde chache, ikakatwa kisha ukatumwa ujumbe mfupi wa maandishi kutoka kwenye simu hiyo ukiwa na neno moja linalohoji 'nani?'

Licha ya mwandishi kujitambulisha na kueleza dhamira ya kumpigia simu kutaka kupata ufafanuzi kuhusu kutoonekana kwake bungeni, alipopigiwa tena, simu hiyo iliita pasina kupokewa na hata kuwapo mrejesho wenye majibu ya kilichoulizwa na Nipashe kwa mbunge huyo.

Ndugai amekuwa Spika wa Bunge la Tanzania tangu Novemba 2015 hadi Januari 6, mwaka huu, ilipotangazwa kuwa amejiuzulu kwa hiari yake mwenyewe. Alikuwa Naibu Spika kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 wakati wa uongozi wa Spika Anne Makinda.

HABARI KITAIFA

# Bunge laanika maeneo ya hatari maambukizi VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, imebaini ongezeko la maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) kwenye mikoa ya Geita na Mwanza huku ikisema sababu kubwa ya ongezeko hilo ni ukosefu wa elimu na upatikanaji duni wa kondomu kwenye maeneo ya mialo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati imetaka kampeni maalum zianze kwenye mikoa ambayo ina maambukizi zaidi ya kiwango cha kitaifa cha asilimia 4.7 ikiwamo Geita na Mwanza.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Toufiq, aliyasema hayo bungeni juzi alipokuwa akiwasilisha maoni ya kamati hiyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2022/23.

Alisema kamati imebaini kuwa hali ya maambukizi ya VVU bado iko juu kwa mkoa wa Geita ambao una asilimia 6.4 na Mwanza kutoka asilimia 4.7 mwaka 2011/12 hadi asilimia 7.2 mwaka 2016/17, ikilinganishwa na hali ya maambukizi kitaifa ya asilimia 4.7.

"Kamati inaona iko haja ya Mamlaka husika kuweka nguvu zaidi katika mikoa hii ili kupunguza maambukizi mapya," alisema.

Pia alisema katika baadhi ya mialo ambayo kamati ilitembelea, imebainika kuwa elimu kuhusu Ukimwi bado haijawafikia ipasavyo, hivyo watu wengi hawachukui tahadhari ya kujikinga na maradhi hayo.

"Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo katika mapambano dhidi ya UKIMWI na Kifua Kikuu kwa wavuvi, kiwango kidogo cha upimaji wa VVU katika mialo na kambi za wavuvi kutokana na ugumu wa mazingira ya shughuli za uvuvi,"alisema.

Pia alisema kuna tatizo la upatikanaji wa Kondomu katika maeneo ya mialo, kiwango kidogo cha uelewa kuhusu Sera, Sheria na wajibu kwa waathirika na uhaba wa rasilimali za kuwasaidia waathirika wa VVU katika maeneo ya uvuvi.

"Kamati inaziomba mamlaka husika kuhakikisha zinatoa elimu ya UKIMWI katika maeneo haya na si kusubiri ujio wa Kamati ya Bunge ndipo watembelee maeneo husika," alisema.

Kadhalika, alisema Kamati imebaini kuwa wafungwa na mahabusu wanaotumia dawa za kufubaza virusi (ARV) wanapewa chakula cha aina moja tu ambacho ni ugali na maharage kila siku hali ambayo inafanya wazidi kudhoofika kiafya kwa kuwa dawa wanazotumia ni kali na zina nguvu sana.

"Ipo haja ya Serikali ya kuhakikisha chakula bora kinatolewa kwa WAVIU waliopo magerezani ili kuimarisha hali yao ya lishe,"alisema.

Hata hivyo, alisema Kamati hiyo inashauri fedha zinazopitishwa na Bunge kwa ajili ya mwitikio wa Ukimwi zitolewe kwa wakati ili kutokwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa kipindi husika.

Alihimiza elimu kuhusu unyanyapaa na ukatili wa kijinsia iendelee kutolewa kwa jamii ili kuondoa hofu ya upimaji lakini pia kupunguza maambukizi kutokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake.

TAHADHARI GEREZANI

Toufiq alisema moja ya tatizo lililopo kwenye magereza nchini ni msongamano wa wafungwa na mahabusu na kushauri Mamlaka husika zione namna ya kuhakikisha msongamano huo unapungua ili kupunguza kuenea kwa ugonjwa wa Kifua Kikuu.

"Kamati ilielezwa kuwa wapo baadhi ya wafungwa na mahabusu ambao wanaingia magerezani wakiwa wameambukizwa Kifua Kikuu, magereza huwapima wanapoingia lakini ipo changamoto ya maeneo ya kuwatenga ili wasiambukize wenzao kutokana na msongamano uliopo ambao kwa kiasi kikubwa umekuwa unachangia maambukizi kuenea kwa kasi,"alisema.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiweka shada la maua kwenye jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Spika wa Bunge la Uganda, Jacob Oulanyah, wakati wa kuaga katika viwanja vya Kololo, jijini Kampala, nchini Uganda juzi. Oulanyah, alifariki dunia Machi 20, 2022 nchini Marekani, alipokuwa akipatiwa matibabu. **PICHA: BUNGE**

# Samia, Mwinyi waongoza dua

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana aliongoza hitima ya kumwombea dua Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume, iliyofanyika Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Zanzibar.

Hitima hiyo, pia ilihudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali akiwemo Rais mstaafu wa Zanzibar wa awamu ya sita, Dk. Amani Abeid Karume na Makamu wa Rais wa Tanzania, Philip Mpango.

Wengine ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, viongozi wa vyama vya siasa na viongozi wa dini. Hitima hiyo pia ilikuwa miongoni mwa maadhimisho ya Siku ya Mashujaa ilitanguliwa na dua ya ufunguzi kutoka kwa Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ihad Mussa Salum na Quran tukufu iliyosomwa na Ustadh Abdulrahim Twalib na kuhitimishwa na Sheikh Salim Juma Faki.

Baada ya hitma hiyo, Sheikh Khamis Abdulrahman, Mjumbe wa Baraza la Maulamaa Zanzibar alitoa mawaidha na kumwelezea marehemu mzee Karume kuwa alikuwa kiongozi aliyepigania maendeleo ya wananchi wa Zanzibar na kumwombea Mwenyezi Mungu ampe makazi mema peponi.

Pia Sheikh Khamis alisema kumwombea dua mtu aliyetangulia mbele ya haki ni wajibu kwa kila Mwislamu.

Aliongeza kuwa miongoni mwa mambo mengi mazuri aliyoyafanya Karume ni pamoja na kuweka misingi mizuri ya taaluma kwa kujenga na kuweka jiwe la msingi la Chuo cha Kiislamu kilichoko Mazizini Zanzibar mwaka 1972, ambacho kimetoa wataalamu pamoja na maulamaa mbalimbali ambao wengine hivi sasa wako ndani na nje ya Tanzania wakitoa elimu waliyoipata chuoni hapo.

Hitima hiyo ilifuatiwa na uwekaji wa mashada ya maua katika kaburi la Karume. Waliweka maua ni Dk. Mwinyi, Rais Samia na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Tanzania, Jenerali Venance Mabeyo kwa niaba ya wakuu wa vikosi vya ulinzi Tanzania.

Wengine ni Balozi mdogo wa India Zanzibar, Bhagwant Singh, aliyewawakilisha mabalozi wenzake nchini, Balozi Ali Karume kwa niaba ya familia ya Karume na Mzee Ramadhan Nzori kwa niaba ya wazee. Pia katika tukio hilo, ilisomwa dua na sala vilivyoongozwa na viongozi wa dini katika kaburi la Karume lililoko pembezoni mwa Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui. Mufti wa Zanzibar, Sheikh Omar Kabhi, alisoma kwa niaba ya Waislamu, Padri Stanley Lichinga Katibu Mkuu Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar alisoma kwa niaba ya Wakristo na Nikhil Mahraja Joshi Kandka kwa niaba ya Wahindu.

Aidha, wake wa viongozi wakiongozwa na Mama Mariam Mwinyi walihudhuria katika hitima hiyo pamoja na mjane wa Karume, Mama Fatma Karume na viongozi wengine wanawake wa kitaifa wakiwamo mawaziri, wabunge, wawakilishini na wake wa viongozi wastaafu na wananchi.

Aprili 7, 1972 Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume, aliouawa na wapinga maendeleo na jana ilitimia miaka 50 tangu kutokea kwa tukio hilo.


NICOL
The Economic Shield of the Nation

National Investments PLC
50 Mirambo Street
3rd Floor, Mirambo House
P.O. Box 7465
Dar Es Salaam
**Phone:** +255 22 2111399/0733006177
**WhatsApp-** 0682 720 679
**E-mail:** invest@nicol.co.tz

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU MAALUMU KWA WANAHISA WA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL)**

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu Maalumu wa Wanahisa wa National Investment PLC (NICOL) utafanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), Block 10 Mtaa wa Shaaban Robert, Dar es Salaam pia kwa njia ya Mtandao siku ya Jumamosi tarehe **30 Aprili, 2022 saa 4.00 asubuhi**. Usajili wa Wanahisa utaanza kuanzia saa 2:00 asubuhi.

Agenda ya Mkutano Itakuwa Maalumu Kuteua Wakurugenzi wa Bodi ya National Investment PLC (NICOL)

**MAELEZO MUHIMU:**

i. Mwanahisa anaetarajia kuhudhuria mkutano ni lazima kuwasilisha nyaraka zifuatazo: nakala ya cheti cha Hisa (Depository Receipt) pamoja na Kitambulisho cha Taifa au kitambulisho cha mpiga kura au pasipoti.

ii. Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura, ikiwa hawezi kuhudhuria kwa sababu yoyote ile, anayo haki ya kuteua mwakilishi au wakala kuhudhuria, kuzungumza, na, katika kura ya maoni, kupiga kura badala yake na mwakilishi huyo si lazima awe mwanahisa wa Kampuni.

iii. Fomu za uwakilishi zitapatikana katika ofisi ya NICOL au kwa kutembelea tovuti ya NICOL **www.nicol.co.tz**. Fomu za uwakilishi zinapaswa kutumwa ili kufikia ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni au ofisi ya Katibu wa Kampuni angalau masaa 48 kabla ya muda uliowekwa wa kufanya mkutano au zinaweza kutumwa kwa njia ya barua pepe **invest@nicol.co.tz**, au kwa njia ya **WhatsApp 0682 720 679**.

iv. Wanahisa wanaotaka kuhudhuria mkutano mtandaoni wanashauriwa kujiandikisha mapema/kujisajili mtandaoni kabla ya wakati. Maelezo ya kuingia kwenye mtandao yatatumwa kupitia simu yako ya mkononi.

v. Tarehe ya Kufungwa Daftari la Wanahisa wanaostahili kushiriki mkutano itakuwa Jumatano tarehe 27 Aprili 2022.

**Taarifa za Hisa**

Tunapenda kuwafahamisha Wanahisa wetu wote ambao hawajapata kulipwa magawio yao ama suala lolote kuhusu hisa, ama kubadili taarifa za hisa, wanaombwa kuwasiliana na wakala wetu wa daftari la hisa CSDR kupitia **+255746160516/677070414**, barua pepe: **registrar@csdr.co.tz** au unaweza kutembelea ofisi za CSDR zilizopo jengo la Kambarage, Ghorofa ya 2, Dar Es Salaam.

**KWA IDHINI YA WAKURUGENZI**

**______________________________**

**Adv. Benjamin Mwakagamba**
**Katibu wa Kampuni**
**Aprili 5, 2022**

HABARI KITAIFA



Mkufunzi, Aman Vahaya wa shirika lisilo la kiserikali la RLABS-Tanzania, akitoa mafunzo ya elimu ya biashara na kilimo kwa vijana wanaoishi katika mazingira magumu ambao ni wanufaika wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) kutoka kata tatu za Ihanu, Luhunga na Mdabulo, wilayani Mufindi, mkoani Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Taharuki yaibuka mafuta kuzagaa baharini

**Na Romana Mallya**

TAHARUKI ilizuka jana kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi eneo la Feri baada ya meli isiyofahamika kumwaga mafuta jamii ya petroli na wananchi kuyasomba kwa kutumia madumu.

Mashuhuda wa tukio hilo waliambia Nipashe kuwa tukio hilo lilitokea juzi alfajiri na baada ya mafuta hayo kuonekana ufukweni, wananchi walianza kuyachota na kuyaweka kwenye madumu.

Mfanyabiashara katika soko la Feri, Rashid Abdallah, alisema baada ya mafuta hayo kuonekana, vijana walichukua madumu na kuanza kuyachota.

"Mafuta yalionekana ufukweni sasa vijana walipopata taarifa wakaanza kuyachotea kwenye vidumu. Wakati wakiendelea kuchota ndipo polisi wakafika eneo hili na kuyachukua madumu yaliyokuwa na mafuta na kuyapakia kwenye magari yao. Hawakukamata mtu, walichukua tu madumu ya mafuta na kuondoka nayo na hapa wakaimarisha ulinzi," alisema.

Hata hivyo Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ilala, Canute Msacky, alisema baada ya kupata taarifa walifika eneo la tukio na kuwakamata watu sita pamoja na madumu makubwa matano na sita madogo yakiwa yamejazwa mafuta hayo.

Dereva wa bodaboda, Omary Kikweti, ambaye anaegesha pikipiki yake eneo la Feri, alisema walianza kusikia harufu kali ya mafuta ndipo wakaona watu wakikimbilia eneo hilo la ufukweni kulikokuwa kumetapakaa mafuta na kuanza kuyachota.

"Mafuta haya yalionekana kwa wingi wakati bahari ikiwa imejaa. Yaani vijana walikuwa wanayaweka kwenye vidumu, wengine madumu ya maji.

"Harufu yake ilikuwa kama mafuta ya dizeli ila hatujajua yalikotoka tumeshangaa tu kuyaona ufukweni, vijana walikuwa wanayachota ili wayauze kama mafuta mengine yanayouzwaga kwenye vidumu.

Baada ya tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ngw'ilabuzu Ludigija, alifika eneo hilo na kuwatahadharisha wananchi kuwa makini na ununuzi wa mafuta ya kidumu kuanzia sasa.

Ludigija alisema mpaka wakati huo bado walikuwa hawajafahamu ni meli ipi ambayo imemwaga mafuta hayo na tayari wameshatoa maagizo kwa mamlaka mbalimbali kuanza kuchunguza athari za mafuta hayo.

Alisema baada ya kupokea taarifa ya kuwapo kwa mafuta hayo mara moja alimwagiza Mkuu wa Upelelezi kwenda eneo la tukio.

"Ukanda wote huu wa bahari kwa sasa nyinyi ni mashahidi kuna mafuta yanaelea juu na kwa hali ilivyo baada ya Mkuu wa Upelelezi kufika kwenye ukanda huu aliwakuta baadhi ya wananchi wakiwa wanayachota na kuyaweka kwenye madumu.

"Kama ambavyo mlivyotangaziwa na uongozi wa soko la feri, katika kipindi hiki tusitumie maji yale ya mafuta kwa sababu bado mamlaka zetu hazijafanya uchunguzi na kutupa taarifa sahihi ya madhara ambayo yanaweza kusababishwa na mafuta hayo," aliwaeleza wananchi.

Alisema wanaendelea kuwasiliana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ili wachukue sampuli za maji hayo ili kujua madhara yanayotokana na mafuta hayo.

**KAULI YA NEMC**

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema wanatarajia kuanza uchunguzi wa tukio hilo Jumatatu ijayo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na wanaoingiza mafuta ili kubaini aliyefanya uchafuzi huo wa mazingira.

Alisema wamejaribu kuzungumza na baadhi ya waliowahisi lakini wamekataa kufanya uchafuzi huo.

"Hapo nyuma tuliwahi kupiga faini kampuni kadhaa lakini bado hali inajitokeza. Tumewataka wenye mabomba ya mafuta wayakarabati au kuweka mapya, tutakapompata aliyefanya uchafuzi huu atapewa adhabu kubwa," alisema.

Alisema mafuta yanapomwagwa kwenye bahari husababisha athari kwa viumbe hai, mikoko pamoja na wadudu wanaoirutubisha kufa kutokana na kukosa oksijeni.

## Mawaziri EAC wapendekeza bajeti ya dola mil. 91 mwaka 2022/2023

**Na Benny Mwaipaja,** ARUSHA

Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) limetoa mapendekezo ya bajeti ya jumla ya dola za Marekani milioni 91.6 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kati ya fedha hizo, dola za Marekani milioni 37.5 zinatarajiwa kutolewa na wadau wa maendeleo. Mapendekezo hayo yametolewa kwenye Mkutano Maalum wa 47 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya hiyo uliofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya Jumuiya hiyo, jijini Arusha.

Akizungumza kuhusu Mkutano huo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema kuwa Bajeti inayopendekezwa imezingatia kubana matumizi na kuelekeza fedha nyingi kwenye miradi ya maendeleo ya Jumuiya hiyo.

Mapendekezo ya Bajeti ya Jumuiya hiyo inayoundwa na nchi sita wanachama, ikiwemo Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Sudani Kusini kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ni sawa na Bajeti ya mwaka wa fedha uliopita 2021/2022 na yamebaki hivyo kutokana na changamoto inayopitiwa na Nchi Wanachama katika kukabiliana na madhara ya UVIKO-19.

Baraza hilo limependekeza kuwa kiasi cha dola za Marekani milioni 54.1 kitumike kwa ajili ya mihimili ya Sekretarieti ikiwamo Mahakama ya Afrika Mashariki, Bunge la Afrika Mashariki na Taasisi zake ikiwemo Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EASTECO) na Tume ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC). Taasisi nyingine ni Tume ya Kiswahili (EAKC), Tume ya Utafiti wa Afya (EAHRC) na Mamlaka ya Ushindani ya Jumuiya hiyo (EACA); dola za Marekani 644,219 ni kwa ajili ya Baraza la Vyuo Vikuu Afrika Mashariki (IUCEA) na dola za Marekani 465,500 zitaelekezwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria (LVFO).

Aidha, Baraza hilo Maalum la Mawaziri limependekeza Bajeti ya mwaka 2022/2023 igharamie utekelezaji wa miradi ndani ya Jumuiya, ikiwemo, awamu ya pili ya Ujenzi wa Makao Makuu ya Baraza la Vyuo Vikuu Afrika Mashariki (IUCEA), Matengenezo ya Meli ya Utafiti katika Ziwa Victoria ijulikanayo kama RV Jumuiya, Ujenzi wa Awamu ya Pili ya Makao Makuu ya Tume ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) na Kuwezesha zoezi la uangalizi wa Uchaguzi Mkuu nchini Kenya.

## Shabiby aja na mbinu kudhibiti bei ya mafuta

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Gairo, Ahmed Shabiby (CCM), amesema kuna haja serikali kuruhusu wafanyabiashara mmoja mmoja kuagiza mafuta nje ya nchi, akiamini ndiyo njia sahihi ya kukabiliana na kupaa kwa bei ya nishati hiyo nchini.

Amesema kwamba utaratibu wa sasa wa kuagiza mafuta kwa pamoja ni tatizo kwa kuwa hautoi nafasi ya ushindani wa biashara miongoni mwa wafanyabiashara wa mafuta.

Shabiby aliyasema hayo juzi bungeni jijini hapa alipochangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake.

Alisema kuwa serikali ikiruhusu kampuni binafsi zilete mafuta, bei ya nishati hiyo itashuka, akisisitiza kuwa serikali inapaswa kubaki kuangalia bei ya ukomo haivukwi.

"Wanasema 'ukiruhusu wafanyabiashara mmoja mmoja aagize mafuta, watakwepa ushuru', jamani meli zote zinashusha kwenye mita, hamuwaamini TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania)? Ile mita imekufa mara ngapi? Imekufa mara nyingi zaidi kipindi hiki kuliko zamani.

"Serikali haiwezi kutoa kodi kwenye mafuta, ikitoa kodi kwenye mafuta, nchi hii haina dawa, haina mishahara, hatuwezi kutoa kodi, lazima kodi iwapo kwenye mafuta.

"Watanzania wa sasa wana akili, kukiwa na wizi wanajua kwamba hapa kuna tatizo, kama kuna 'dili' wanajua hapa hili ni 'dili'. Nilionya mapema hapa bungeni kwamba ununuzi wa mafuta kwa pamoja utaleta shida, sasa imekuwa ni moto.

"Nimeshasema na ninarudia kusema, ilikuja kampuni moja hapa ya India, ikashusha bei ya mafuta kwa kiwango kikubwa lakini ikapigwa vita, ikazuiwa mtu binafsi kuleta mafuta.

"Matokeo yake ni kwamba ukishanunua mafuta kwa pamoja, wote mnakuwa na bei moja, nani atashusha? Hakuna tena ushindani kwenye mafuta, yule jamaa wa India ikabidi auze kampuni yake kwa watu waliopo hapa.

"Kuna kampuni zinauza mafuta kwa robo ya bei ya dunia. Ukimruhusu mfanyabiashara alete mafuta, atayapata ya bei rahisi, nchi hii inatumia lita milioni 400 kwa mwezi, lakini ukishasema tu hapa, utasikia wanasema 'huyu Shabiby atakuwa mwizi wa mafuta huyu' wakati wezi mko huko huko, ndiyo majambazi," alisema.

**MATREKTA MABOVU**

Mbunge huyo pia aliitaka serikali kuchukua hatua za kisheria dhidi ya walioingiza nchini matrekta aliyoyaita mabovu, akisisitiza kuwa yamesababisha hasara kwa wakulima.

"Serikali imeleta matrekta mabovu, sijawahi kuona trekta linakatika katikati, yote ni mabovu, mmewatia umaskini hawa wakulima. Aliyeagiza yale matrekta ashtakiwe, hapa kuna wizi. Tujue nani kayaleta na ana mkataba gani," alisema.

Mbunge huyo pia aliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi ya maji jimboni kwake, huku akiwatahadharisha mawaziri kuwa 'Rais Samia Suluhu Hassan hapendi sifa, bali ufanisi wa kazi'.

Mbunge wa Makambako, Deo Sanga (CCM), aliitaka serikali kuhakikisha inamaliza kero zinazokwamisha mradi wa Mchuchuma na Liganga, pia kuongeza posho za madiwani nchini.

# Wanahabari waidai Quality Group mil. 232/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDISHI wa habari waliokuwa waajiriwa katika Kampuni ya Quality Group Limited, wameiburuza mahakamani kampuni hiyo, wakishinikiza kulipwa Sh. milioni 232.

Tangazo la kuitwa mahakamani kwa wawakilishi wa kampuni hiyo, lilitolewa jana kwenye gazeti moja (sio Nipashe), likiwataka kufika mahakamani Aprili 20, mwaka huu saa tatu asubuhi, mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, E. M. Kassian.

"Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi au wawakilishi wenu wanaotambulika kisheria, basi maombi hayo yatasikilizwa bila uwepo wenu," lilieleza tangazo hilo.

Mwakilishi wa waandishi 22, Joseph Lugendo, alithibitisha kuiburuza mahakamani kampuni hiyo kudai kiasi hicho cha fedha kilichotokana na Tuzo ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Temeke, iliyotolewa Juni 24, mwaka 2019.

Lugendo alidai tangu walipopata hukumu hiyo, wamekuwa wakiomba kampuni hiyo itekeleze Tuzo hiyo, lakini haikuwahi kufanya hivyo.

Alidai wamefikia uamuzi wa kuiburuza kampuni hiyo mahakamani kwa mara nyingine ili kuomba mahakama imkamate Mkurugenzi wake, Yusufu Manji, kwa kuwa ndiye aliyesaini barua za kusitisha ajira zao kinyume cha taratibu.

Alidai kabla ya tangazo hilo, waliomba mahakama kutoa hati ya kumuita Manji na wawakilishi wa kampuni hiyo kortini, iliyotolewa Februari 24, mwaka huu, lakini wanasheria waliokuwa wakiiwakilisha kampuni hiyo na Mkurugenzi huyo, walidai hawana mkataba tena na mteja wao huyo wa zamani.

Lugendo alidai baada ya kushindwa kumpata Manji, wala wawakilishi wa kampuni hiyo, walirudi mahakamani Machi 29, mwaka huu, kuomba kutangaza wito huo gazetini, ili wawakilishi hao na/au Manji, wafike kortini kueleza sababu za kutolipa malipo hayo.

"Miongoni mwa waandishi ninaowawakilisha, wapo wanaodai Shilingi milioni tatu na wengine chini ya hapo. Kwa utajiri wa kampuni hiyo na Manji, hatuoni sababu za kushindwa kulipa madai yetu," alidai Lugendo.

Kwa mujibu wa hukumu hiyo ambayo gazeti hili limepata nakala yake, hati ya kupinga kuondolewa kazini kwa waandishi hao iliwasilishwa kwa usuluhishi, ambao ulishindikana na baadaye Oktoba 24, 2017, ilihamishiwa kwa ajili ya uamuzi.

Ilidaiwa mbele ya mwamuzi kwamba waandishi hao waliajiriwa katika kampuni hiyo katika nafasi mbalimbali kwa nyakati tofauti, lakini wote walisitishiwa kazi siku moja ya Sepemba 19, mwaka 2017.

Hukumu hiyo inasema, waandishi hao walidai kuajiriwa na Kampuni ya Quality Group, lakini mikataba yao ilisitishwa kwa barua na kampuni hiyo na aliyesaini barua za kusitisha mikataba hiyo ni Yusuf Manji mwenyewe.

Miongoni mwa waandishi hao, wapo waliodai mikataba yao ya ajira ilichukuliwa na mwajiri na walilazimika kuwasilisha barua ya kusitishwa kazi na hati ya kupokea mshahara kuthibitisha kuajiriwa kwao.

Hukumu hiyo imeeleza kwamba kwa kuwa mlalamikiwa hakufuata utaratibu wa haki katika kusitisha mikataba hiyo, waandishi hao wana haki ya kupewa sehemu ya mishahara iliyokuwa imebaki katika mkataba wao wa kazi, ambayo jumla yake ni Sh. milioni 232.

# Wadau sekta ya elimu wafunzwa ubunifu

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imetoa mafunzo ya utekelezaji wa awamu ya pili ya programu ya 'Lipa kulingana na matokeo katika sekta ya elimu' kwa wadau wa sekta hiyo.

Lengo la mafunzo hayo yaliyoratibiwa pia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ni kuwawezesha kuwa wabunifu na kuweka mikakati ya kutekeleza mipango kazi yao.

Kamishna wa Elimu wa wizara hiyo, Prof. Lyambene Mutahabwa, alifungua kikao hicho juzi mkoani Dar es Salaam, kilichowakutanisha wadau hao wakiwamo maofisa elimu wa mikoa, msingi, sekondari pamoja na wadhibiti wakuu ubora wa shule wa kanda na wilaya.

Alisema awamu ya pili ya programu hiyo, itasaidia kuhakikisha kuwa vipaumbele zaidi vya sekta ya elimu vinatekelezwa kwa kuzingatia mipango na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka husika.

Aliongeza kuwa, programu hiyo iliyojikita katika maeneo sita utekelezaji wake utaiwezesha serikali kupata fedha kupitia hiyo na kuifanya iweze kufikia malengo yake ya kutoa elimu bora kwa watoto wa kitanzania.

"Mafunzo haya yamekuja wakati muafaka kwani yatatoa fursa kwa wadau wa elimu hususani wasimamizi na watendaji wa elimu katika ngazi ya kanda, mikoa na halmashauri kufahamu kwa kina kuhusu programu hiyo," alisema Mutahabwa.

Alisisitiza pia kupitia mpango huo, utawawezesha washiriki hao kujadili vigezo vya kupata fedha ili kuwa na uelewa wa pamoja na kuweka mikakati thabiti ya kusaidia mamlaka za serikali za mitaa kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa vigezo ili kupata fedha.

Alisema utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango huo, umesaidia kuleta mafanikio makubwa ikiwamo kujenga utamaduni wa kutumia rasilimali zilizopo kwa ufanisi katika kutekeleza malengo ili kuleta maendeleo endelevu.

Pia, fedha zitakazopatikana kutokana na programu hiyo, zitatumika kutekeleza vipaumbele katika elimu pamoja na kuchochea utekelezaji wake ili kuwezesha upatikanaji wa fedha zaidi.

## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together, we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA WA MIZANIA ULIOKAGULIWA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2021 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2020 |
|---|---|---|---|
| A | **ASSETS** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 832.82 | 1,279.03 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 9,467.90 | 3,824.46 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 35,070.14 | 30,890.00 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 529.37 | 621.27 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 141.50 | 32.00 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 36,356.91 | 34,455.39 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 51,115.39 | 48,424.85 |
| | 12 Mali Nyingine | 1,069.55 | 917.50 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| | 14 Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 726.37 | 1,123.04 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **135,309.96** | **121,567.55** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 36,430.00 | 33,084.50 |
| | 18 Amana za Wateja | 56,654.61 | 48,164.40 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0.00 | 0.00 |
| | 20 Amana Maalumu | 0.00 | 0.00 |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0.00 | 0.00 |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0.00 | 0.00 |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,533.45 | 2,064.56 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0.00 | 0.00 |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0.00 | 0.00 |
| | 27 Dhima Nyingine | 453.03 | 628.52 |
| | 28 Madeni | 0.00 | 0.00 |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **95,071.09** | **83,941.98** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **40,238.87** | **37,625.57** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 1,279.37 | 41.35 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 3,516.20 | 3,095.93 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,613.31 | 1,658.29 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 0.00 | 0.00 |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0.00 | 0.00 |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,238.87** | **37,625.57** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 6,760.70 | 10,219.56 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 1,632.81 | 1,319.31 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 437.92 | 364.15 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | 0.00 | 0.00 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 29.74% | 30.95% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.17% | 2.71% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 55.42% | 60.03% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 37.78% | 39.83% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 90.96% | 94.10% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | 14.57% | 16.24% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | 11.30% | 12.55% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2021

| | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2021 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2020 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 9,635.81 | 8,750.58 |
| 2 Gharama za Riba | 3,237.67 | 3,292.98 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6,398.15** | **5,457.60** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0.00 | 0.00 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 73.77 | 201.25 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **945.99** | **850.83** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 152.73 | 174.73 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 792.38 | 676.10 |
| 6.3 Gawio | 0.00 | 0.00 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0.87 | 0.00 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **3,529.20** | **3,524.73** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 1,376.29 | 1,295.53 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 33.92 | 30.77 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 2,118.99 | 2,198.43 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,741.16** | **2,582.45** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,127.85 | 924.16 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,613.31** | **1,658.29** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 80 | 51 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 80 | 51 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.09% | 1.46% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 6.70% | 4.49% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 48.05% | 55.87% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.52% | 5.27% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2021 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2020 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 2,613.31 | 1,658.29 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | 0.00 | 0.00 |
| | Hasara katika mali | 402.48 | 894.96 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | -2,690.54 | -14,001.25 |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | 11,835.71 | 11,349.44 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 715.81 | 1,671.43 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 761.66 | -189.86 |
| | Kodi iliyolipwa | -1,168.25 | -891.19 |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **12,470.18** | **491.82** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | 0.00 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | -5.82 | -58.41 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | 0.00 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | -2,005.73 | -11,676.21 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **-2,011.55** | **-11,734.62** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(Malipo ya dhima kukodishwa)-IFRS 16 | -254.15 | -230.25 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **-254.15** | **-230.25** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **10,204.48** | **-11,473.04** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa mwaka | 36,896.83 | 48,369.87 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa mwaka** | **47,101.31** | **36,896.83** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI ILIYOKAGULIWA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2021

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 4,754.21 | 41.35 | - | - | **37,625.56** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,613.31 | - | - | - | **2,613.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,238.02) | 1,238.02 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **6,129.50** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,238.87** |
| **Mwaka Uliopita 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 2,308.69 | 828.58 | - | - | **35,967.28** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,658.29 | - | - | - | **1,658.29** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 787.23 | (787.23) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **4,754.21** | **41.35** | **-** | **-** | **37,625.56** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2021

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 23-03-2022 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 23-03-2022 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 23-03-2022 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| RAJABU SELEMAN KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 23-03-2022 |
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 23-03-2022 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 23-03-2022 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchunguzi MSD wa upotevu dawa ufanyike haraka

**JUZI,** Rais Samia Suluhu Hassan, aliagiza Wizara ya Afya kuchunguza haraka mifumo inayotumiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kwa kufuatilia dawa tangu zinatoka hadi kufika kwa mtumiaji.

Agizo hilo limetolewa ikiwa ni takribani wiki moja tangu alipoweka bayana kwamba taasisi hiyo inapaswa kusukwa upya, ikiwa ni pamoja na kufumua uongozi mzima na kuweka watu wapya.

Rais alitoa agizo hilo baada ya kupokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ambayo pamoja na mambo mengine, ilionyesha upungufu katika utendaji kwenye taasisi hiyo.

Kila kikao cha bunge halikosekani swali kwenda Wizara ya Afya, kutaka kujua lini serikali itahakikisha dawa na vifaa tiba vinapatikana, huku wakitoa mifano ya wananchi kutakiwa kununua dawa kwenye maduka binafsi, kwa kuwa hakuna dawa kwenye zahanati, kituo cha afya na hospitali.

Wapo wanaokwenda kutibiwa wanaandikiwa dawa, lakini hawajui pa kuzipata kwa kuwa wanatakiwa kutembea umbali mrefu kuzitafuta kwa gharama kubwa, na mbaya zaidi zinapatikana kwenye maduka binafsi kuliko serikalini.

Katika kukabili hali hiyo, Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli, aliagiza MSD kuwa na maduka yake karibu na hospitali ili wananchi wapate huduma kirahisi kwa zile ambazo haziko kwenye orodha ya kugharamiwa na serikali.

Ni muhimu kufanya uchunguzi wa mifumo ili kubaini wapi dawa zinapotelea, kwa kuwa siyo jambo la karibuni bali limeongelewa kwa miaka mingi linahitaji kufanyiwa kazi kubwa.

Pia, kuna wakati Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliagiza maduka yaliyopo umbali wa mita 500 kutoka kwenye hospitali kuondolewa, kwa kuwa kuna uwezekano wa kutoroshwa dawa kutoka hospitalini.

Licha ya serikali kueleza kuwa maboresho makubwa yamefanyika kuhakikisha hakuna upotevu wa dawa,lakini bado hazifiki kwa watumiaji kama inavyotakiwa na imekuwa kawaida kuandikiwa dawa za kwenda kununua.

Ni muhimu serikali ikafanya uchunguzi wa kina kwa kuwa yapo malalamiko mengi ya kukosekana kwa dawa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali, kwa kuwa badala ya wananchi kunufaika wachache ni wanufaikaji wakubwa jambo ambalo ni hatari sana.

Ni kawaida kukuta majengo mazuri na wakati mwingine yana hadi vifaa tiba vizuri lakini mgonjwa anaambiwa hakuna dawa, anatakiwa kwenda kununua kwenye maduka binafsi ambayo mengi yamejengwa karibu na maeneo ya tiba.

Kwa sasa maduka ya dawa baridi na dawa muhimu yanamea kwa wingi ambayo yanakuwa na kila aina ya dawa, lakini kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma hazipatikani.

Kama ambavyo CAG amependekeza kufumuliwa kwa taasisi hiyo na sasa Rais ameona umuhimu wa kufanya uchunguzi wa mfumo wa dawa tangu inatoka MSD, basi ni muhimu sana ili wananchi waridhike kuwa asilimia 80 ya dawa zinazoelezwa kusambazwa zimewafikia.

Hotuba ya wizara hiyo mwaka 2021/22 ilisema serikali kupitia MSD hununua, hutunza na kusambaza aina 2,545 za dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Kati ya hizo, dawa aina 1,865 ni dawa zilizo katika utaratibu wa Miradi Msonge na aina ya dawa 680 ni dawa muhimu.

Aidha, dawa za aina 312 ndizo zimeainishwa kuwa ni dawa muhimu na za kipaumbele cha wizara kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinapatikana nyakati zote katika MSD.

Ilisema katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, hali ya upatikanaji wa aina hizo 312 katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ilifika asilimia 75.6 na katika maghala ya MSD ni asilimia 21 ikilinganishwa na hali ya upatikanaji wa dawa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/20, ulikuwa ni asilimia 80 katika vituo vya kutolea huduma na asilimia 56 kwa MSD.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Shughuli za kiuchumi ziendelee, ila tuzingatie mwongozo wa UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

**TANZANIA** imeendelea na utaratibu wake wa kukabiliana na UVIKO-19 kwa kutofungia ndani wananchi bali wanaendelea na shughuli za kiuchumi huku wakizingatia mwongozo wa kujikinga na ugonjwa huo.

Tofauti na nchi nyingine ambazo ziliwahi kusimamisha shughuli zote tangu ugonjwa huo uliposambaa katika nchi mbalimbali duniani kama njia ya kukabiliana na ugonjwa huo, kwa Tanzania ilikuwa ni tofauti.

Wizara ya Afya ilitoa mwongozo wa kujikinga na ugonjwa huo ikielekeza wananchi kuendelea na shughuli zao za kiuchumi lakini kwa kuhakikisha wanachukua tahadhari zote za kuepuka UVIKO-19.

Miongoni mwa tahadhari hizo ni kuvaa barakoa, kunawa maji tiririka, kutumia vitakasa mikono, pia kuna kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima kuanzia mitaani, kwenye biashara na hata usafiri.

Pamoja na maelekezo hayo, suala la kuepuka mikusanyiko linaonekana mtihani mgumu hasa kwa wafanyabiashara wadogo, wamekuwa wakirundikana sehemu moja, hali ninayoamini si salama kwao.

Kwa mfano masoko ya Mabibo, Shekilango, Mbezi Luis na mengine ya jijini Dar es Salaam, wafanyabiashara wanaendelea na shughuli za kiuchumi bila tahadhari ya ugonjwa huo, kutokana na jinsi wanavyorundikana.

Ninadhani kwamba, umefika wakati sasa kwa wafanyabiashara wadogo na watu wengine kutambua kuwa kuna haja ya shughuli za kiuchumi kuendelea, lakini kwa kuzingatia tahadhari ya UVIKO-19.

Kwanini? Ni hivi karibuni Wizara ya Afya, ilitangaza kuwapo aina mpya ya kirusi cha UVIKO-19 kilichothibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na kuelekeza wataalamu wa afya kuangalia kama kimeshaingia nchini.

Hatua hizo zinachukuliwa, kutokana na kwamba kirusi hicho, kinajumuisha kirusi cha Delta na Omicron, ambacho kimejiunda na kuwa kirusi kipya cha Omicron BA.1, kimeshathibitishwa kuingia kwenye baadhi ya nchi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema WHO inafanya utafiti wa kufahamu ukali wa kirusi hicho kipya huku wizara hiyo ikiendelea kufanya utafiti wa kuwapo kwa kirusi hicho nchini.

Anawasihi Watanzania kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na kirusi hicho, kwa kuwa watu wengi wakipata chanjo watasaidia kupunguza madhara ya ugonjwa huo utakapothibitika kuwapo nchini.

Binafsi ninaunga mkono kile kinachotangazwa na serikali kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo kuchukua tahadhari zaidi ikiwamo kuzingatia mwongozo na kuchanja, huku shughuli za kiuchumi zikiendelea.

Ikumbukwe Waziri anasema, asilimia 66 ya wanaougua UVIKO-19 waliolazwa hospitalini hawajapata chanjo, ninaamini hali hiyo ni hatari kwa nchi, hivyo ingekuwa vyema tukiungana na serikali kukabili ugonjwa huo.

Pia, ni vyema jamii kuelewa kuwa Tanzania siyo kisiwa kisichofikika bali ina mwingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali, hivyo suala la kujikinga na ujio wa kirusi hicho kipya ninadhani ni muhimu.

Hayo ni vyema nikawakumbusha msemo wa Kiswahili kwamba; 'ukimuona mwenzio ananyolewa, na wewe tia maji', hivyo ni kwamba ingawa kirusi hakijafika nchini, bado ipo haja ya kuchukua tahadhari.

Ninaamini watu wenye afya njema wana nafasi kubwa ya kuchangia katika uzalishaji mali na kukuza uchumi, hivyo kuzingatia mwongozo kutasaidia watu kuwa salama na kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Ninajua kuwa suala la chanjo ni hiari, lakini kufuata mwongozo si hiari bali kinachotakiwa ni utekelezaji tu, kuanzia kunawa maji tiririka, kutumia vitakasa mikono, kuvaa barakoa na pia kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Ninaamini kuwa, iwapo jamii itazingatia mwongozo huo, huku watu wakijitokeza kwa wingi kupata chanjo, itakuwa rahisi kuendelea na shughuli za kiuchumi bila kuhofia ugonjwa wa UVIKO-19.

Kwa ujumla, ninaweza kusema kuwa, Watanzania kuendelea na shughuli za kiuchumi inawezekana, lakini jambo la msingi linalotakiwa ni wao kuzingatia maelekezo yaliyomo katika mwongozo wa UVIKO-19.

## MAONO YA PROF. NGOWI

# Aeleza sifa za mjasiriamali

**Na Jenifer Gilla**

NI dhahiri kuwa marehemu Prof. Honest Ngowi, aliyekuwa Mhadhiri wa Uchumi wa Chuo Kikuu Mzumbe, na mtaalam wa biashara na uchumi kabla umauti kumkuta siku kadhaa zilizopita aliwekeza katika kuwainua wajasiriamali wa aina zote.

Katika moja ya mambo aliyoyafanya ni kutoa elimu katika lugha nyepesi itakayomsaidia mjasiriamali mdogo kujitambua na kufanya mambo yatakayomfanya akue katika tasnia yake.

Moja ya somo ni sifa anazopaswa kuwa nazo mjasiriamali. Ni muhimu kwa kundi hilo kwa kuwa linatoa mwongozo wa namna mwana tasnia anapaswa kuwa ili asitetereke.

Katika kipindi chake alichokiweka kwenye channel yake ya Ngowi TV, mchumi huyo alieleza kuwa ujasiriamali kama njia moja wapo ya kuongeza uchumi inahitaji umakini na kujitambua.

Kwa mujibu wa Prof. Ngowi, ili mjasiriamali awe mahiri anatakiwa awe na uwezo wa kuona fursa za kibiashara.

Anatakiwa awe na uwezo wa kuona vitu ambavyo mwingine hawezi kuviona na asipokuwapo haviwezi kufanyika.

"Mjasiriamali ndiye anayepanga pamoja hizi 'factors of production' (sifa za bidhaa) ikiwamo kuleta vifaa, ili mambo yaweze kwenda katika biashara kwa hiyo anahitaji kuwa na jicho linaloona fursa mbalimbali katika biashara yake," alifafanua.

Sifa nyingine ya mjasiriamali kwa mujibu wa Prof. Ngowi ni awe mtu mwenye uthubutu (take risks). Kwa maana ya kuwa awe na uwezo wa kukabiliana na mambo yasiyo na uhakika. Alifafanua uthubutu ni kuchukua mkopo benki au kwenye vikundi kwa ajili ya kuendesha biashara ambayo mtu hana uhakika kama italipa au la, kuwekeza katika kilimo ambacho hana uhakika kama mvua itanyesha kwa kiwango kinachohitajika na kukuza mazao inavyopaswa.

Aliongeza kuwa katika uthubutu mjasiriamali anatakiwa awe na uwezo wa kufanya uamuzi ambao hautoangusha biashara yake. Alitoa mfano wa mkulima kama anaona kuwa kuna dalili za mvua kutonyesha, aweke miundombinu mingine ya upatikanaji wa maji, na kwa mfanyabiashara anaweza kukata bima ili kama isipolipa asipate hasara kubwa.

Sifa nyingineni kuwa na maono, mjasiriamali anatakiwa awe na uwezo wa kuiona kesho yake siku ya leo.

Mambo mengi yanayofanywa na wajasiriamali yangekuwa yanafanywa kwa ajili ya leo yasingefanyika ni malengo ya baadaye. "Mjasiriamali asiyekuwa na njozi hawezi kuwa mzuri, tunachosema ni kwamba wajasiriamali wazuri ni wale wanaochekwa kwa kufikiria mambo ambayo wengine wanayaona kuwa ni ndoto, lakini matokeo huja kuonekana siku nyingi sana zijazo," alisema Prof. Ngowi.

Alitoa mfano kuwa mjasiriamali anatakiwa awe mtu ambaye amepanda mti ambao hana uhakika kama kivuli chake atakikalia au matunda yake kuyala. Yule anayehofia kupanda mti kwa kudhani kuwa ataondoka kabla matunda yake hajayala, hawezi kufanikiwa.

Alisema mjasiriamali mzuri ni anayekubaliana na hali aliyonayo wakati huo huku akijijenga kufika juu zaidi ya hapo. Alitoa mfano kuwa mjasiriamali anapolalamika kuwa hawezi kufanya ujasiriamali kwa sababu hana fedha anakuwa anakosea kwa sababu moja ya sababu za ujasiriamali ni kutafuta pesa.

Vilevile, Prof. Ngowi alisema kuwa mjasiriamali anapaswa kuwa mtu mwenye fikra chanya. Kwa sababu katika tasnia hiyo kuna mambo mengi ya kukatisha tamaa, bila ya kuwa na mtazamo chanya ni rahisi kukata tamaa.

# NACTVET: Vyuo 52 ruksa sasa kudahili wanafunzi kwa mkupuo

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), limetoa orodha ya majina ya vyuo 52 nchini, vilivyoruhusiwa kufanya udahili wa wanafunzi kwa mkupuo msimu wa Machi kwa muhula wa mwaka wa masomo 2022/2023.

Limesema kwamba idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwa utaratibu huo kwa miaka ya nyuma iliwezesha wanafunzi kati ya 30,000 hadi 40,000 kudahiliwa, likibainisha idadi hiyo itapungua mwaka huu kwa sababu ya baadhi ya vyuo vilivyokuwamo kwenye mpango huo ikiwamo kada ya afya kutodahili awamu ya Machi.

Mkurugenzi wa Uthibiti, Ufuatiliaji na Tathmini, Dk. Jofrey Oleke, aliiambia Nipashe jana, iliyotaka kuondoa sintofahamu kutoka kwa baadhi ya wazazi au walezi, wakielezea kupokea ujumbe mfupi wa maandishi kuhusu watoto wao kutakiwa kujiunga na vyuo msimu huo.

"Mwaka huu 'in take' ya Machi udahili wa wanafunzi utapungua tofauti na miaka ya nyuma. Kati ya vyuo hivyo 52 ambavyo tayari vimeruhusiwa kudahili vitaongezeka vichache ambavyo vilichelewa kutuma maombi na wiki ijayo tutaviongeza kwenye idadi. Utaratibu wa miaka ya nyuma ulikuwa unachukua wanafunzi wengi lakini udahili huu umeondoa baadhi," alisema Dk. Oleke.

Kwa mujibu wa taarifa katika tovuti ya baraza hilo, iliyotolewa juzi na Ofisi ya Katibu Mtendaji NACTVET, ilibainisha hayo na kuelezea kwamba kuanzia Aprili 6 hadi Aprili 18, mwaka huu, vyuo hivyo vimeruhusiwa kuanza kufanya udahili huo, ikiwamo wa wanafunzi waliohitimu kidato cha nne mwaka jana.

"Vyuo vinavyohusika kwenye udahili huu ni vile vilivyopata kibali, baraza litavichukulia hatua za kinidhamu vyuo vitakavyokiuka maelekezo hayo. Imebainika kuwa kuna vyuo tayari vinaendelea kufanya matangazo na kupokea maombi ya nafasi za masomo kwa Mkupuo wa Machi, bila kuwa na ridhaa ya baraza.

"Kitendo hiki ni kinyume cha maelekezo yaliyotolewa," ilisema taarifa ya awali iliyotolewa na baraza. Vyuo vitakavyohusika kwenye udahili huu ni vilivyopata kibali kama vilivyoambatanishwa na tangazo hili," ilifafanua taarifa iliyotolewa kwenye tovuti ya baraza hilo.


CRDB BANK

*The bank that listens*

## BOARD MEMBERS VACANCIES

CRDB Bank Plc is a leading commercial bank in Tanzania. Established in 1996, the Bank has grown and prospered over the years to become the most innovative and trusted Bank in the country. The Bank attained an important milestone when it was listed on the Dar Es Salaam Stock Exchange on 17th of June, 2009. CRDB Bank Plc owns Two subsidiary companies - CRDB Bank Burundi S.A. and CRDB Insurance Broker Limited.

The Board of Directors invites applications from suitably qualified candidates to fill five positions of Board Members, three to represent the group of shareholders owning shares below 1% of the share capital of the Bank, one Board Member to represent shareholders owning shares above 1% and below 10% of the share capital of the Bank and one Independent Director elected by all shareholders.

"Independent Director" means a director who- (a) does not hold any executive or management position in the bank; (b) does not have, directly or indirectly, a significant interest in the bank including any parent or subsidiary in a consolidated group with the bank; "Significant interest" means a holding of five percent or more of the voting shares of the bank (c) has not been employed by the bank or its subsidiaries of which he currently forms part in any executive capacity for the preceding three (3) years; (d) is not a member of the family of an individual who is, or has been in any of the past three years, employed by the bank or its subsidiaries in an executive capacity; (e) is not a professional advisor to the bank or its subsidiaries ; (f) is free from any business or other relationship which seems to interfere with the individual's capacity to act in an independent manner; and (g) does not receive remuneration contingent upon the performance of the bank as defined in the Banking and Financial Institutions (Internal Control and Internal Audit) Regulations 2014;

The names of qualified candidates will be submitted to the Annual General Meeting for election.

**( https://crdb.tiny.us/MEMARTS )**

**Expertise and Knowledge Requirements**

In line with Section 5(2) of the Banking and Financial Institutions Act (Corporate Governance) Regulations, 2021 candidates for the Board of Directors positions should have the expertise and knowledge in the following academia: Banking; or Finance; or Accounting; or Auditing; or Law; or Economics.

**Skills Requirements**

Taking into account the current market practice, technological development and growth in digital banking, the following skills are required for the Board of Directors Positions: Mergers and acquisition; or IT systems, data science, cyber security, trade and project finance, engineering and insurance.

**Roles of Board of Directors**

1. Determine the Bank's vision, mission and values aimed at providing continuity and legal existence of the Bank.
2. Continuously monitor and evaluate the Bank's strategy to achieve the vision and mission and ensure the Bank survives and thrives.
3. Govern the Bank by broad policies and objectives, formulated and agreed with Managing Director. Such policies and objectives shall aim at ensuring that:
   - 3.1 Procedures and practices are in place to protect the Bank's Assets and reputation;
   - 3.2. The Bank complies with all relevant laws, regulations and codes of best practices; and
   - 3.3. The technology and systems used in the Bank are adequate to properly run the Bank for it to compete through efficient use of its assets, processes and human resources.
4. Monitor risk identification and its management so as to enhance shareholder value in the long run.
5. Select and appoint the Managing Director to whom the responsibility of managing the Bank shall be delegated. The Directors shall review and evaluate the Managing Director's performance regularly.

**Mode of Application**

1. Any CRDB Bank shareholder who wishes to be elected as Board member must submit an application letter, curriculum vitae, certified copies of relevant academic and professional certificates and awards, two passport size photographs, certified copies of the last page of their passports, and letters of recommendation from 3 references and declaration of indebtedness to banks.
2. Notification of receipt of application and other details will be sent to all applicants upon receipt of the applications. Applications must be received by **4.00 p.m.** on **Monday, 11th April, 2022**.

**CRDB strongly encourages women to apply**

The contact for communication is:

**The Secretary**
**CRDB Bank Plc Headquarters**
**Plot No 25 and 26 Ali Hassan Mwinyi Road & Plot No. 21 Barack Obama Road**
**P. O. Box 268, 11101 Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel. no. 022 - 2219566**
**E-mail: shares_unit@crdbbank.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**J. B. Rugambo**
**COMPANY SECRETARY**

**28th March, 2022**

# Machinga wapewa mkopo mil. 105/- kuinua mitaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imefanikiwa kutatua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu baina yao na wajasiriamali wadogo kwa kuwapatia eneo la biashara la kituo kidogo cha mabasi (CDT) na mkopo wa Sh. milioni 105 ili kuwainua kimitaji.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo Anderson Msumba, aliyabainisha hayo jana wakati alipotembelewa na madiwani wa Mkoa wa Kilimanjaro waliofika kujifunza namna ya ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa miradi yenye tija kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri.

Alisema, awali wajasiriamali wadogo walikuwa wakifanyakazi zao kiholela kwa kuranda randa mitaani, kupanga biashara zao pembezoni mwa barabara na kando ya maduka ya wafanyabishara wakubwa hali ambayo ilikuwa ikisababisha wafanyabiashara kupiga kelele na kuibuka migogoro.

Aidha, alisema wamewapatia eneo la kituo kidogo cha mabasi CDT kwa ajili ya kufanyia biashara zao bila kubughudhiwa na kila mmoja amejenga kibanda chake cha biashara na eneo hilo lina machinga, mama ntilie pamoja na mawakala wa mabasi.

"Katika eneo hili kuna wajasiriamali wenye sifa ya kupata mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri na wale wasio kuwa na sifa waliungana na kutengeneza Chama cha kuweka na kukopa (Saccoss), ambapo tuliwapatia Sh. milioni 105 ambazo wanakopeshana ili kujiinua kimitaji," alisema Msumba.

Mwenyekiti wa wajasiriamali wa CDT Baroza Ezekiel alisema, katika eneo hilo kuna jumla ya wajasiriamali wadogo 175 na wote wana vibanda kwa mikopo iliyotolewa na halmashauri na ile iliyotolewa na Saccos na sasa wanaendelea na urejeshaji ili kuwapatia fursa wengine kukopa na kuinua mitaji yao.

Naye Diwani wa Kata Masama Kusini Halmashauri ya Hai, Cedrick Pangani alisema, halmashauri yao imekuwa ikiwakopesha wajasiriamali fedha za mikopo, lakini wakati wa urejeshwaji wanawatuma madiwani kwenye kuwadai wajasiriamali hali ambayo fedha zimekuwa zikipotea katika vikundi.

Pangani alisema, anashangaa kuona Halmashauri ya Manispaa ya Kahama inawapatia mikopo mikubwa ya namna hiyo wajasiriamali na wakati mwingine kuwakopesha zana za kufanyia kazi ili nao waondoke na tatizo la urejeshaji wa mikopo watakuwa wanapata vifaa vya kazi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti ALAT wa Kilimanjaro, Saleh Mkwizu, aliipongeza Manispaa ya Kahama kwa kuwatumia wajasiriamali kwa fursa ya kuongeza mapato ya ndani kwa kuwapatia eneo, kuwapanga na kuchukua kodi.

Mkwizu alizitaka Halmashauri za Mkoa wa Kilimanjaro kuiga utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wajasiriamali na kuwapatia mikopo ya kuiinua mitaji yao ili hapo baadaye waje wanufaike na mapato kutoka kwa wajasiriamali hao watakaokuwa wamewapanga kwenye maeneo tengevu.

# Kongani ya viwanda kuajiri watu 500

**Na Joseph Mwendapole**

MRADI wa Kongani ya Viwanda ya Kamaka (Industrial Park), unaojengwa Kibaha mkoani Pwani, unatarajia kuwekeza Sh. bilioni 60 na kutoa ajira za moja kwa moja kwa watu 5,000.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, wakati yeye na ujumbe wake walipotembelea mradi huo eneo la Mlandizi.

Alisema mradi huo unatarajia kujengwa kwa awamu tatu huku awamu ya kwanza ikihusisha miundombinu ya barabara, maji, umeme, uzio na majengo na imekamilika kwa asilimia 55.

Dk. Kazi alisema mradi huo utaongeza mapato ya serikali kwa kuongeza wigo wa kodi lakini pia ujenzi wa zaidi ya viwanda 200 kwenye eneo hilo utarahisisha upatikanaji wa bidhaa mbalimbali.

"Huu ni mradi wa kujivunia sisi Watanzania kwa sababu utatengeneza fursa nyingi za ajira.

Ni mradi mkubwa sana na TIC itaendelea kusaidia kutatua changamoto ili wakamilishe haraka," alisema.

Pia alisema hata kabla ya mradi huo kukamilika, zaidi ya watu 300 wameshaajiriwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za ujenzi wa mradi huo ambao alisema unakwenda kwa kasi inayoridhisha.

"Kilichotuvutia zaidi ni kwamba hawa watu walipata cheti cha usajili Juni, mwaka jana na wakaanza ujenzi Oktoba. Sasa kwa utaratibu wetu mwekezaji anapaswa kutoa taarifa miezi sita anaendeleaje. Sasa huyu anakwenda kwa kasi ambayo hatukuitarajia, " alisema.

Dk. Kazi alisema mradi huo uko kwenye eneo la fursa kwa sababu uko karibu na treni ya kisasa ambapo mwekezaji ataweka bandari kavu kwa ajili ya kurahisisha shughuli ya kusafirisha bidhaa zitakazozalishwa na wenye viwanda maeneo hayo.

"Kwa muda mrefu sasa umekuwa wito wa serikali na Rais Samia Suluhu Hassan kuhamasisha watu wajenge kongani za viwanda na sisi TIC tumeahidi kwamba tutawahudumia kwa spidi kubwa sana ili watu wapate ajira na serikali ipate kodi na sisi tuunaahidi hatutapoa kwenye suala hili," alisema

Yusuph Manzi, mmoja wa Wakurugenzi wa Kamaka, alisema mradi huo unaonyesha dhamira ya dhati kwa Watanzania kuunga mkono serikali katika ujenzi wa kongani za viwanda.

Alisema mradi huo utakamilika kwa muda uliopangwa na ni matarajio yao mradi kwamba utachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya mkoa wa Pwani na taifa kwa ujumla.

Mradi huo, alisema uko kwenye eneo la ukubwa wa ekari 1,000 na awamu ya kwanza ya ujenzi inatarajia kukamilika Desemba, mwaka huu.



Meneja miradi wa Shirika la Investing in Children and Strengthening their Societies (ICS) mkoani Shinyanga, Sabrina Majikata (kushoto), akitoa mafunzo ya malezi bora ya watoto kwa mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali mkoani humo juzi, kwa ajili ya kuwajengea ujuzi wa kutoa elimu hiyo kwa wananchi wanapokuwa wakitekeleza miradi yao kwa jamii. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bulembo 'amvaa' Mpina, ataka achukuliwe hatua

**Na Gwamaka Alipipi**

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdallah Bulembo, amemuomba Makamu Mwenyekiti wa chama hicho bara, Abdulrahman Kinana, kumhoji na kumchukulia hatua za kinidhamu Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina kwa madai ya kwenda kinyume na maadili ya chama.

Bulembo amesema hatua ya Mpina kuongea hadharani akimshutumu Waziri wa Nishati, January Makamba, kwamba uamuzi alioufanya wa kuondoa tozo ya Sh. 100 kwenye lita ya mafuta ulikuwa ni wa uhujumu uchumi, vyombo vya uchunguzi vifanye kazi yake haikuwa kauli nzuri.

Juzi, Mpina akizungumza na waandishi wa habari alisema Waziri wa Nishati, Makamba hakufuata utaratibu wa kisheria wa kuondoa tozo ya Sh. 100 kwa lita ya mafuta, hakupata baraka kutoka bungeni na mchakato wake ulikuwa batili.

Mpina alisema tozo hiyo ya mafuta ipo kisheria katika bajeti ya serikali ya mwaka 2021/22, Waziri Makamba alivunja Katiba ya nchi na hakuwa na mamlaka ya kuondoa tozo hiyo iliyopitishwa na Bunge.

Pia, Mpina alitaka Waziri Makamba kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kushtakiwa kwa uhujumu uchumi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuanza kumhoji waziri huyo kwa kosa la kuingizia hasara Taifa Sh. bilioni 30 kwa mwezi Machi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Bulembo alisema: "Mpina ni mbunge wa CCM, CCM ina vikao vya ndani vya chama ambavyo vinatumika kuwekana sawa pindi mmoja anapokwenda ndivyo sivyo, sasa yeye (Mpina) kwa nini hakutumia vikao vya chama hadi anazungumza hadharani."

"Yeye ni mbunge, angezungumzia suala hilo ndani ya Bunge na siyo nje. Namuomba Kinana aanze na Mpina kwa kitendo alichokifanya cha kumshambulia Waziri Makamba hadharani, huko ni kukosa maadili."

Bulembo ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM, alisema suala la kuondolewa tozo ya Sh. 100 kwa lita ya mafuta lilishatolewa ufafanuzi na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alitangaza kuirejesha, Mpina hakupaswa kulizungumzia tena suala hilo.

Aliongeza kuwa hata suala la kuchelewa kukamilika kwa mradi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere, Mpina hakupaswa kulizungumzia kwa sababu Rais Samia alishalizungumzia kuwa limechelewa na litakamilika mwaka 2024.

"Kinana hili suala lazima alichukulie hatua. Mpina hawezi kuivua nguo CCM hadharani angetumia vikao vya chama kuzungumza hayo aliyoyasema. Ninaamini kile alichokisema Mpina, Kinana amekisikia na amekiona na atachukua hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Katiba ya CCM," alisema Bulembo.

Alisema Mpina ni mbunge wa muda mrefu, ni mwanachama wa CCM mzoefu ambaye anafahamu miiko na taratibu za chama na sehemu sahihi ya kuzungumzia na kuwa kitendo alichokifanya kitawafundisha wanachama wadogo wa CCM kuzungumza kiholela pasipo kufuata utaratibu uliowekwa kichama.

# DC awashauri wadau kuunga mkono juhudi watoto kupata elimu bora

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, amewataka wadau wa maendeleo kuunga mkono juhudi za awamu ya sita kuhakikisha kila mtoto anapata elimu bora.

Hayo aliyasema jana wakati wa kupokea msaada wa viti na meza kwa ajili ya Shule ya Sekondari Tangazo, mifuko ya saruji 20 kwa ajili ya Shule ya

Kambarage pamoja na kukabidhi kiti cha magurudumu (wheel chair) kutoka Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Alisema mwanafunzi anatakiwa apate elimu bora na ni lazima asome katika mazingira yanayostahili na yenye mahitaji yote muhimu, ili aweze kupata ufaulu mzuri katika mitihani yake.

"Natoa rai kwa wanafunzi wote kuwa hii imeanza toka mwaka 2020 kuwa mwanafunzi anayefanya vizuri katika mitihani yake ya kidato cha nne kwa kufikia ufaulu wa daraja la kwanza anapata kiasi cha milioni moja na hilo nataka lianzie kwenu,"amesema Kyobya

Meneja wa NBC Tawi la Mtwara, Editha Mwakatobe, alisema lengo la msaada huo ni kuondoa changamoto ya elimu kwa wanafunzi.

Pia aliwataka wazazi ambao hawajawapeleka watoto wao shuleni wafanye hivyo haraka na kuagiza jeshi la polisi kuwakamata wazazi wote ambao hawajawapeleka shule na kueleza wamewapeleka wapi watoto hao.

Aidha, benki hiyo ilikabidhi viti 50 na meza 50 kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Tangazo, iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, ambapo ilijengwa na kuanza kudahili wanafunzi mwaka 2021.

Pia ilikabidhi mifuko ya saruji 20 kwa Shule ya Msingi Kambarage iliyopo katika Kata ya Shangani West, ili kuweza kufanya ukarabati wa madarasa.

Benki hiyo ilimkabidhi kiti cha magurudumu Mzee Abeid Yusufu, ambaye alikuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi wa Sekondari ya Mtwara Technical kwa kuwashonea viatu vyao bila malipo yoyote.

"Miezi kadhaa tulishaanza na leo tumeendelea tena katika shule hizi mbili, ila naamini tutaendelea kutoa msaada huu kwa wanafunzi, ili waweze kusoma kwenye mazingira mazuri na kupata elimu bora," alisema Mwakatobe.

Baadhi ya walimu wa Shule ya Sekondari Tangazo na Shule ya Msingi Kambarage waliushukuru uongozi wa NBC kwa kuona umuhimu na kuwajali watoto wao ili waendelee kupata elimu bora.

# Misitu hekta 3.9 zapotea kila mwaka kwa uharibifu

**Na Salome Kitomari**

ZAIDI ya hekta milioni 3.9 za misitu hupotea kila mwaka Afrika kutokana na uharibifu wa mazingira, hali inayotakiwa kuchukuliwa hatua za makusudi kulinda rasilimali hiyo muhimu kwa maisha ya watu.

Hayo yalibainika hivi karibuni wakati wa maswali ya waandishi wa habari kwenye semina kwa wataalamu wa mazingira na misitu kutoka nchi mbalimbali Afrika, ambao walikutana kushirikishana uzoefu na taarifa kuhusu changamoto na fursa zilizoko kwenye utunzaji na uhifadhi endelevu wa misitu katika wakati wa mabadiliko ya tabianchi.

Ofisa Mkuu wa Jukwaa la Misitu Afrika (AFF), Prof. Godwin Kowero, alisema ripoti ya hali ya msitu Afrika ya mwaka 2020 iliyotolewa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ilionyesha nchi nyingi za Afrika zina asilimia zaidi ya 10 ya misitu katika ardhi yao, huku nchi tano zikiwa na zaidi ya asilimia 70.

Naye, Ofisa Programu Mwandamizi wa AFF, Prof. Marie Louise Avana, alisema ripoti hiyo ya FAO inaonyesha kuwa Afrika inaongoza kwa uvunaji wa misitu kwa kiwango cha milioni 4.41 cha misitu iliyopotea kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 20200.

Pia, inakabiliwa na wadudu sumbufu na kwamba asilimia 37 ya misitu ya Afrika imeathiriwa na wadudu huku asilimia 29 ni moto, na kwamba nchi za Kusini mwa Afrika kiwango cha upotevu ni asilimia 0.62 ikifuatiwa na Afrika Magharibi asilimia 0.59 kwa mwaka.

"Tunawasihi wadau wa misitu kuongeza jitihada za kuelimisha umma kwa kueleza umihimu wa bidhaa na huduma zinazotolewa na misitu kwa binadamu na mazingira kwa ujumla,"alisema Prof. Avana.

Aidha, alisema kumekuwa na jitihada za kutunza na kuendelea misitu ambazo hazitoshelezi kwa kuwa haziendani na kasi ya uharibifu ambayo inazidi kuongezeka.

Naye, Profesa Labode Popoola, alisema ni lazima serikali za Afrika zije na mikakati ya kuzuia ukataji wa misitu unaoongezeka kila siku kwa serikali kuweka kipaumbele kwenye sekta hiyo muhimu kwa maendeleo endelevu.

Kuhusu kazi zilizofanywa na AFF, Prof, Kowero alisema ni taasisi ya wadau inayoongozwa na mahitaji ya watu na maendeleo ya mazingira kwenye misitu na miti nje ya raslimali za misitu.

Alisema hayo husaidia kuchambua changamoto zinazokabili pande zote na kuangalia fursa zinazoendelea kujitokeza katika kufikia mahitaji ya watu huku wakitumia rasilimali misitu kwa muundo endelevu.

Alisema kongamani hilo lilijadili matokeo ya kazi kuu tatu, kati ya nyingi zilizofanywa na AFF; nazo ni juu ya namna ya kupanua na kuendeleza misitu, kulinda na kuisimamia kwa uendelevu, kwa kwenda sambamba na malengo ya misitu ya dunia; pamoja na uwezo wa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara Afrika wa kukuza au kupanda mbegu na miche ya miti ambayo itatosheleza mahitaji yao yanayotegemea miti na misitu.

Aidha, mengine ni uwezo wa bara la Afrika kulinda uwekezaji kwenye misitu ya kupandwa na asili dhidi ya wadudu na magonjwa kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa ujuzi wa ufuatiliaji wake na uwepo wa miundombinu duni kusaidia uchunguzi wa kimaabara.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Mohamed Mtesa (kulia), akikabidhi moja ya magodoro 40 kwa Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mihumo, yaliyotolewa msaada na Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka, kwa ajili ya shule hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara zasaka suluhu mgogoro wa ardhi makazi ya wazee Dar

**Na Sabato Kasika**

BAADHI ya wizara zimekutana kujadili kwa kina ili kuutafutia ufumbuzi wa kudumu, mgogoro wa ardhi unaoendelea kwenye makazi ya wazee wasiojiweza yaliyopo Nunge Kigamboni Dar es Salaam.

Wizara za kisekta zilizokutana ni za Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Katiba na Sheria na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Akizungumza na waandishi wa habari kabla ya wizara hizo kujifungia ndani kujadili mgogoro huo, Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, alisema waliovamia ardhi ya makazi ya wazee hao wanatakiwa kuondoka mara moja.

"Eneo hilo linatakiwa kuachwa kwa ajili ya malengo yaliyopangwa ambayo ni kulea wazee wasiojiweza, wanatakiwa kuzingatia sheria za matumizi ya ardhi waache mtindo wa kuvamia ardhi," alisema Dk. Chaula.

Dk. Chaula alisema serikali imekuwa ikitenga ardhi kwa matumizi mbalimbali ikiwamo kuwatunza wazee wasiojiweza kama ilivyo kwa makazi ya Nunge, lakini akashangaa kuona watu wakivamia na kujenga nyumba.

Awali akitoa taarifa ya uvamizi huo, Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii anayeshughulikia Wazee, Tullo Masanja, alisema kuwa Wizara imefanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha mgogoro huo unamalizika, lakini wavamizi wameendelea kusonga katika makazi hayo ya wazee wasiojiweza.

"Hadi sasa takriban nusu ya ardhi kwa ajili ya makazi ya wazee yenye ukubwa wa ekari 50 imevamiwa ingawa hatua mbalimbali za kuwaondoa zimefanyika ikiwa ni pamoja na kuwataka kuondoka kwa hiari yao," alisema Masanja.

Akifafanua zaidi, Masanja alisema uvamizi huo ulianza mwaka 1981 baada ya familia aza watu nane kudai kuwa eneo hilo ni lao na kutaka walipwe na kwamba uvamizi huo umeendelea kupanuka.

"Madai yao si ya kweli kwani makazi ya wazee wasiojiweza yalianza miaka ya 70 na wao wameanza kuvamia mwaka 1981 na hawana ushahidi wowte wa kuonyesha kuwa ni maeneo yao," alisema.

Alisema, serikali imeendelea kufanya jitihada mbaimbali ikiwamo kuweka mabango kuonyesha ni eneo la serikali, lakini wavamizi wanayaondolea, na kwamba walishawapa siku 45 waondoke na kwamba bado wapo.

"Pamoja na hayo, niseme tu kwamba, huu si mgogoro mkubwa kwani waliopo ni Watanzania, hivyo kikao hiki kinatafuta njia bora ya kuumaliza kwa kushirikisha wadau mbalimbali,"alisema.

Kamishna wa Ardhi, Mathew Nhonge, alisema haki itatendeka na kwamba watahakikisha mgogoro huo unamalizika ili kila kipande cha ardhi kitumike kwa mujibu wa matakwa ya sheria za mipango iliyowekwa na serikali.

"Ikumbukwe kuwa, linakuja suala la maeneo ya serikali, lazima tujue kuwa maeneo haya sio ya kukimbilia na kuvamia kwani unatenda kosa la jinai na hautovumilika katika hilo," alisema Nhonge

Makazi ya wazee wasiojiweza ya Nunge, ni miongoni mwa makazi 14 ya wazee yanayosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa lengo la kuwahudumia na kuwalea wazee hao.

# Euro milioni 5.4 kutekeleza mradi miundombinu majitaka

**Na Mohamed Saif-**
MWANZA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) inatarajia kutekeleza ujenzi wa mradi wa miundombinu ya majitaka na usafi wa mazingira wenye thamani ya Euro milioni 5.3 kwa lengo la kupunguza uchafuzi wa Ziwa Victoria.

Mradi huo unafadhiliwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania, Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya Maendeleo ya KfW na Umoja wa Ulaya (EU) chini ya uratibu wa LVBC kupitia programu ya pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria (LVB-IWRM).

Hayo yalibainika hivi karibuni jijini Mwanza katika kikao kilichoshirikisha wadau kutoka MWAUWASA, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria na ujumbe kutoka KfW ukiongozwa na Meneja anayesimamia miradi Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika, Martina Maurer.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Leonard Msenyele, alisema ufadhili huo uliweka vipaumbele mbalimbali vyenye nia ya uhifadhi wa mazingira kwa miji inayozunguka Ziwa Victoria kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Mradi utawezesha ukarabati na upanuzi wa mtandao wa majitaka kwa takriban kilomita 14.4 sambamba na kuunganisha kaya 1,600, uboreshaji vituo vya kusukuma majitaka na ununuzi wa vifaa vya usimamizi wa mfumo wa majitaka yakiwamo magari ya kuondoa taka majumbani," alibainisha Mhandisi Msenyele.

Alisema ufadhili huo unafuatia ushirikiano madhubuti kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mataifa ya nje. "Wengi ni mashahidi, mnaona namna ambavyo Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan anavyoweka msisitizo kwenye suala la ushirikiano wa kimataifa," alisema Mhandisi Msenyele.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaleta manufaa makubwa kwenye utunzaji wa mazingira hususan kupunguza uchafuzi wa Ziwa Victoria.

Kiongozi wa ujumbe huo, Maurer alisema mradi umelenga kupunguza uchafuzi wa Ziwa Victoria hususan unaotokana na utiririshaji ovyo wa majitaka.

Akielezea kuhusiana na ziara yao hiyo ya siku moja mkoani Mwanza, Maurer alisema imelenga kujionea eneo la mradi na kujadili namna bora ya utekelezwaji wake.

"Tunatarajia kujifunza mengi kuhusu namna mnavyotekeleza miradi yenu husan ya utunzaji wa mazingira (uondoshaji wa majitaka) sambamba na kujadili changamoto zinazowakabili kwenye utekelezaji wa miradi kwa ufumbuzi wa pamoja na pia kubaini maeneo zaidi tunayoweza kushirikiana," alisema Maurer.

Kaimu Meneja Ufundi wa MWAUWASA, Mhandisi Salim Lossindilo, alitaja maeneo yatakayonufaika na mradi huo ni Igogo, Kirumba, Mwaloni, Nyamanoro, Kitangiri na Pasiansi.



Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (kulia), akibadiliashana mawazo na Wabunge wa Viti Maalumu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Halima Mdee (kushoto) na Ester Bulaya, walipokutana katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwaka mmoja wa Samia ulivyoiboresha Mwanza

**Vitus Audax na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKOA wa Mwanza umemwaga sifa lukuki kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza siku 365 za uongozi wake kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo tangu alipoingia madarakani.

Akizungumza na watendaji wa serikali na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoani Mwanza, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alisema katika kipindi hicho, miradi ya elimu, afya, maji, barabara na huduma za kijamii zimeboreshwa.

Alisema kuwa katika sekta ya elimu Mkoa wa Mwanza umepatiwa zaidi ya Sh. bilioni 4.5 ambayo kwa sasa inatumika katika ujenzi wa vyuo viwili vya ufundi katika Wilaya za Ukerewe na Kwimba.

"Katika sekta ya elimu tumepatiwa fedha ambazo zimesaidia kujenga jumla ya vyumba vya madarasa 985, ofisi za walimu 51, maabara 11, matundu ya vyoo 81,nakala za vitabu milioni 1.87 kwa ajili ya shule za msingi na wanafunzi wenye mahitaji maalum, tumepatiwa Sh. bilioni 4.5 ambayo kwa sasa inatumika kujenga vyuo vya ufundi viwili katika wilaya za Kwimba na Ukerewe," alisema.

Aliongeza kuwa mkoa huo umepatiwa pia zaidi ya Sh. bilioni 28.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya elimu.

Katika sekta ya afya alisema kuwa Sh. milioni 10.8 imetolewa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za wilaya, Sh. bilion 3.75 fedha za tozo kwa ajili wa vituo vya afya 10, Sh. bilioni 4.9 zilitolewa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma katika Hospilali ya Rufani ya Kanda ya Bugando na kusaidia utolewaji wa huduma za kibingwa katika hospitali hiyo.

Gabriel alisema katika sekta ya maji MWAUWASA imetengewa Sh. bilioni 88.1 ambapo hadi kufikia Machi, imepokea Sh. bilioni 29.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya usambazaji wa maji ambao umefikia asilimia 39, huku RUWASA wakipatiwa kiasi cha bilioni 13 ambapo ilipokea bilioni 11.5, kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini na utekelezaji wake ukifikia asilimia 66.

Aidha, alisema katika kipindi hicho, miundombinu na huduma za kijamii zimeboreshwa katika mkoa na kurahisisha shughuli za usafirishaji na uwekezaji.

## NMB kuendelea kuhudumia jamii

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB Kanda ya Magharibi imesema imeendelea kuwekeza katika kusaidia shughuli za kijamii kama sehemu ya kutekeleza sera yake ya kuwajibika kwenye maeneo inakofanya biashara .

Meneja wa tawi la NMB Kigoma, George Fundi, alisema mwaka jana taasisi hiyo kubwa ya fedha kuliko zote nchini ilitumia takribani Sh. bilioni 2.06 kusaidia kutatua changamoto mbalimbali za kimaisha na kimaendeleo katika maeneo mengi ya nchi.

Alieleza kuwa uwekezaji huo utaongezeka kutoka Sh. milioni 84 hadi Sh. bilioni 2.9. Hii ni baada ya benki hiyo kupata faida ya kihistoria ya Sh. bilioni 290 ambapo ina utaratibu wa kutumia asilimia moja ya kila faida inayopatikana kwa ajili ya kusaidia kutatua kero na changamoto zilizopo katika maeneo yake ya kipaumbele.

Alisema msaada huo unajikita kwenye mambo makuu manne ikiwamo kutoa elimu ya fedha, kuchangia madarasa na hospitali.

Alisema sera yake ya CSR inalenga zaidi kufanya maisha ya wadau wake wote na wananchi kwa ujumla kuwa bora zaidi

Naye Dk George Masasi kutoka Hospitali ya Manispaa ya Kahama, aliishukuru benki hiyo kwa msaada wake kusaidia kupunguza kwa vifo vya kinamama na watoto wachanga wakati wakujifungua kuchangia vifaa ikiwamo vitanda, magodoro, viti vya kubebea wagonjwa na machela.

"Pamoja na kwamba serikali inaendelea kujitahidi kufanya maboresho, changamoto katika mfumo wetu wa afya bado ni nyingi sana kuweza kuzitatua peke yake, kwa hiyo ushirikiano kutoka taasisi kama NMB utasaidia na ni muhimu wakati wote," alisema Dk. Masasi,

Muuguzi mwandamizi Zahanati ya Old Shinyanga , Simon Madangi alisema vitanda na mashuka ya NMB vimeleta ahueni ya kuzuia kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza, huku wangonjwa wakifurahia msaada huo kwa kusema kuwa utaboresha mazingira ya uzazi na kuwahamasisha wajawazito kujifungulia hospitali badala ya nyumbani.

Baada ya NMB kusaidia kupatikana vitanda 10, mashuka 50 na magodoro 100, hospitali hiyo imefanikiwa kuongeza uzazi salama kutoka 10 hadi 80 kwa mwezi.


NMB pia ilisaidia katika sekta ya elimu kwa kutoa vifaa kwa baadhi ya shule ikiwamo Shule ya Sekondari ya Uhuru iliyopo katika Manispaa ya Shinyanga iliyokuwa na madawati 17 tu hapo awali. shuleni hapo kuwa madawati 17 tu.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, Musa Walelo, alisema kwa sasa hakuna tena tatizo la utoro shuleni kwao kutokana na kuwapo kwa vifaa vyote muhimu vya kufundishia .




Ukurasa 12

Mipango aliyoisimika 1964, imedumu kuwa dira inayofuatwa kitaifa hadi leo




Ukurasa 13

Bunge mbashara tutarajie mapya?


# BUFE

IJUMAA APRILI 8, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA





Ukurasa 14

**Naibu Waziri aibua mpango kuwasuka vijana kumiliki uchumi wao**

# Naibu Waziri Masanja atua kwao akitaka wafuge nyuki, asali iwalipe

**Na Anthony Gervas,** Mwanza

UFUGAJI nyuki una faida kubwa kutokana na asali kuwa zao la kibiashara na chakula, ambayo hivi sasa walaji ni wengi.

Unaweza ukatumia kama dawa kumpakaa mtu aliyepata majeraha ya kuungua na maji ya moto au moto.

Wapo wanaotumia kwenye chai ya rangi kama vile kiungo cha sukari,hasa wenye magonjwa ya presha na mengineyo. Pia, sumu na nta zake huuzwa katika masoko mbalimbali na viwandani.

Wananchi wengi wamegundua ufugaji nyuki wa kutumia mizinga ya kisasa na kuvuna asali nyingi kuliko kutumia mizinga ya kienyeji, Tanzania ikiwa na utajiri wa mapori.

Tanzania ni ya pili katika uzalishaji asali, nyuma ya Ethiopia. Mapori yapo mengi ya kufugia, lakini elimu sahihi kwa jamii kuhusu fursa hiyo bado haiko sawa. Soko la asali kwa sasa liko juu, kutokana na matumizi mengi.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

### AFUNGUKA YA KWAKE

Mary Masanja, ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii mzaliwa wa wilayani Magu, Mwanza. Akiwa nyumbani aliwahimiza madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo, kuwahamasisha wananchi katika ufugaji nyuki.

Anasema ufugaji yuki ni mradi wa kibiashara unaoweza kumuingizia mwananchi kipato kikubwa, kuinua uchumi wake kutokana na soko kubwa.

"Madiwani mnatakiwa kubuni mbinu ya kuhamasisha wananchi waanzishe miradi ya ufugaji wa nyuki, ili kuvuna zao la biashara,mimi mwenyewe naibu waziri nimeanzisha mradi wa ufugaji nyuki,anasema Masanja.

Masanja anawashauri viongozi wilayani humo waanze kufikiria uwekezaji mkubwa wa ndani ikiwamo majengo makubwa kibiashara, kama madiwani hao walivyopendekeza kuanzisha mji wa Kisesa wilayani humo.

Anasena Wizara ya Maliasili na Utalii inaingiza kipato kikubwa na wananchi wanapaswa kutumia fursa kwa ufugaji huo, ili wanufaike kimaisha.

### VIKUNDI VYA WANAWAKE

Naibu Waziri huyo, anawasisitiza wanawake kuanzisha vikundi vya ufugaji nyuki, akitolea mfano msitu wa Hifadhi Ndogo ya Taifa ya Sayaka, wanaweza kuitumia kuweka mizinga ya kufuga, kwani ni msitu mzuri.

Anaeleza kuwa wanawake wana fursa kubwa ya kufanya biashara au uwekezaji, hivyo vikundi ambavyo hata yeye atavipa ushirikiano ni muhimu kuhakikisha vinasonga mbele katika mradi huo.

Anasisitiza soko la asali lipo katika maeneo mengi nchini kutokana na umuhimu wa matumizi yake na wafugaji nyuki wamekuwa wengi zaidi, baada ya kuzifahamu fursa zilizopo.

### ELIMU INAYOTAKIWA

Ni maono ambayo yanahitaji elimu zaidi ya jamii kuhusu fursa zitokanazo na ufugaji wa nyuki na tija inayotokana na kuvuna asali, utunzaji mazingira na misitu ya kufuga, upandaji miti na utengenezaji mizinga bora ya kisasa wakati wa kufuga.

Inaelezwa hivi sasa, viongozi wengi wa serikali wameanzisha miradi ya mfano kwa wananchi wanaohisi hauwafai kwa matarajio yako mbioni

### UPANDAJI MITI KITAIFA

Waziri Masanja akawakumbusha kwamba Machi 21 mwaka huu 2022 ni siku ya kupanda miti kitaifa, hivyo Wilaya ya Magu ni miongoni mwa wapandaji miti, ili kurudisha uoto wa asili katika ardhi yake kwenye maeneo mbalimbali.

Anawahimiza wananchi na viongozi wengine kushiriki zoezi hilo la upandaji,akitaka Magu iwe ya kijani na kivutio kikubwa cha watu wanaofika na kujionea manzari nzuri iliyopo.

Wilaya ya Magu mpaka sasa ina fursa nyingi pamoja na vivutio ikiwemo Makumbusho ya Kageye -Kayenze ambayo ni sehemu ya utalii yanayotarajiwa kufufuliwa kama kivutio cha utalii ambayo hivi sasa bado ni chakavu.

Makumbusho hayo yanatokana na eneo la kumbukumbu ya magofu ya wakoloni ambao ilikuwa kambi yao ya kuwakusanya watu weusi na kuwapeleka utumwa,(manamba) ambayo yako kando mwa Ziwa Victoria.

Eneo hilo ni kivutio kikubwa linalotembelewa na watalii wa ndani kutoka jiji la Mwanza na maeneo mengine jirani,endapo yakiboreshwa yataingizia halmashauri hiyo kipato.

Wananchi wazalendo tuna deni la kuvipenda vitu vyetu vya ndani,kufahamu manufaa yake,badala ya kupenda vya kigeni ,ndiyo maana makumbusho hayo hayakuendelezwa na kuachwa yakichakaa kuwa mapori ya kulala popo na ndege wengine.

# Mipango aliyoisimika 1964, imedumu kuwa dira inayofuatwa kitaifa hadi leo

- Ililenga kujiweka sawa, ilivyopangwa ikageuka kamusi kuu
- Mikakati uchumi, uhusiano, muundo serikali haujasogea

**Na Peter Orwa**

KATIKA historia Tanzania inabebwa na mambo kadhaa, yanayobaki nguzo ya kumbukumbu.

Ingawaje miaka mingi inafahamika kihistoria kwa wengi, hata hivyo mwaka 1964 kwa wengi haujaingia katika kumbukumbu zao. Unabaki kuwa mwaka wa kihistoria Tanzania.

Itakumbukwa ni mwaka ambao kisiasa Tanzania iliamua mambo makuu matatu, nyuma yake ikabeba matokeo makubwa ya kiuchumi yenye uhai hadi sasa.

Ni zama Tanganyika na Zanzibar ziliungana kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huku katika sura hiyo ya kisiasa ukaundwa mfuko wa chama kimoja cha siasa uliodumu kwa miaka 28, kabla ya kurejea mfumo huria kama awali.

Kuwapo mfumo huo ndio uliokaribisha dhana 'Chama kushika hatamu', kwa namna ya mawazo na maelekezo yanaanzia chama tawala - TANU (hata CCM) na kisha yanapelekwa serikalini kutekelezwa, chama kikiendelea na nafasi ya usimamizi.

Aidha, 1964 ni mwaka ulioundwa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) inayodumu hadi sasa kwa ufanisi mkubwa wa utendaji ndani ya muda katika muundo wake kukaundwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Hali kadhalika, hadi mwaka 1964 serikalini maofisa wake wengi walikuwa wa kigeni hasa Waingereza, jambo lililofanya kuwapo haja ya mageuzi ndani ya utumishi wa umma kuziba nafasi.

### MPANGO 1964-1965

Haja ya kufanikisha hayo yote, ndiko kwa mara ya kwanza kukaundwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 1964 hadi 1969 ilipokuwa unahitimishwa.

Ni mpango ambao maudhui yake wakati huo yameendelea kutumika katika mipango iliyofuata mabadiliko makubwa, inapewa sura inayoendana wa wakati husika.

Kulikuwapo pengo kubwa katika nyenzo na mikakati ya maendeleo, kuifanya Tanzania na watu wake wajitegemee, ikiwamo elimu, afya, miundombinu, biashara, uchumi na nyenzo za maendeleo, sambamba na kujaza nafasi kwenye utumishi wa umma.

Mahitaji ya kutekelezwa wakati huo yaliangalia mahitaji ya msingi ya kuanzia na ndipo hapo katika eneo la elimu, kukaangaliwa zaidi haja ya kujitosheleza kwa kasi kubwa kwenye elimu ya shule za msingi kuwafikia wananchi waliko ngazi ya vijiji, ikiendana na huduma za afya ya msingi hukohuko.



Watumishi wa Kiwanda cha Nguo Urafiki kazi ya mipango ya awamu ya kwanza nchini. **PICHA: MTANDAO**

> **"Miradi hiyo ikapata ziada ya uwekezaji, pale benki binafsi ya kimataifa iliyotaifishwa kupitia Azimio la Arusha, ikazaa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), mali ya umma.**

Mtazamo wa msingi uliangaza elimu kwa Watanzania wengi ukawafumbua wainuke kifikra na ujuzi. Pia, katika stadi maalumu, mtazamo wa mpango huo chini ya mwassisi Mwalimu Nyerere, aliamua kufanyia kazi upungufu wa watumishi wa umma.

Katika maeneo ya biashara na menejimenti, mara moja akaanzisha ujenzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Dar es Salaam mwaka mmoja baadaye.

Ikumbukwe mwaka 1965, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilizaliwa kisheria kutoka iliyokuwa Benki Kuu ya Afrika Mashariki.

Hali kadhalika, wazo kutoka mpango huo kujaza nafasi ya wataalamu lilizaa Chuo cha Uongozi wa Maendeleo (IDM) Mzumbe, Morogoro miaka sita baadaye kutoka iliyokuwa taasisi ya kuandaa watumishi wa serikali ya mtaa, iliyoundwa mapema mwaka 1953.

Katika kuhitimisha pengo la makazi, mpango kukajengwa nyumba nyingi za kukopesha kuanzia mwaka 1966, chini ya kivuli cha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kwa utaratibu majengo duni ya wakazi yalibomolewa na watu wakajengewa kwa utaratibu wa kulipa taratibu.

Hiyo inashuhudiwa katika miji kama Morogoro na jijini Dar es Salaam, ambako hadi sasa kuna majengo yanayofanana katika makazi ya Temeke, Ilala, Magomeni, Kinondoni na Mwananyamala.

Pia, Rais Nyerere wakati huo aliwekeza kuziba pengo la watumshi na wataalamu wengi kwa kutumia ofa kutoka marafiki kama vile China nchi za Ulaya Mashariki, Urusi (ya USSR), Cuba na watawala nchini wa zamani, Uingereza. Baada ya kati ya miaka mitatu hadi sita, kukashuhudiwa kumiminika wahitimu hasa wa udaktari wengi kutoka China na Russia, ambako chuo kikuu chake Lumumba kikawa maarufu kitaifa.

Vivyo hivyo, wahasibu wengi wakinolewa Uingereza na kurudi na vyeti vya kihasibu kama ACCA na ACA (nchini ikaanzishwa CPA), wanajeshi baadhi na wakaenda kutwaa digirii za kijeshi kutoka Chuo Kikuu cha Soundest

Wanahabari nao baadaye wakaandaliwa fursa kujiendeleza kwa programu maalum ya elimu, hata kwa waliopungukiwa sifa katika Chuo Kikuu cha Cardiff Uingereza.

### UCHUMI NA BIASHARA

Msingi mwingine wa mageuzi makubwa katika uchumi nchini, uliolenga katika mambo kadhaa kama sura mpya uchumi kutoka 'kuzalisha tusichotumia na kutumia tusichokizalisha' hapo ikimaanisha taifa kuhama kutoka uzalishaji malighafi yanayouzwa nje ya nchi na kisha kuagiza bidhaa za kigeni.

Hiyo ilikuwa tafsiri pana ya Mwalimu Nyerere, aliyoona mbali. Kwanza, uzalishaji nchini ungefungua ajira kwa Watanzania wengi, malighafi yao kama pamba na michikichi kuwapatia soko walimaji wote na wafanyabisahara nao kunufaika kwa pamoja.

Katika hatua hiyo ya mpango wa kwanza, ilibeba mtazamo viwanda hivyo kuzalisha bidhaa za matumizi ya msingi, kama vile nguo, vyakula na mafuta ya kupikia.

Hata kinachozungumzwa sasa 'mnyororo wa thamani' kilifanyika kwa hatua ya uzalishaji kuongezea thamani, huku mkulima na mzalishaji wakitegemena katika kinachojulikana kibiashara 'backward and forward linkage'; mzalishaji anahitaji malighafi na mkulima anahitaji bidhaa za kutumia.

Katika kuhitimisha Tanzania hiyo ya viwanda, Rais Nyerere alifanya kazi ya ziada ikiwamo kuwasiliana na nchi rafiki kama China katika kutimiza azma ya kuwekeza katika uzalishaji na huduma na akafanikiwa.

Ni miaka michache tu kukashuhudiwa uwekezaji mkubwa nchini wa viwanda na sura ya kipekee katika viwanda vya nguo kama Urafiki na Kiltex, jijini Dar es Salaam na kukajengwa Chuo Cha Ualimu Chang'ombe.

Ili kuhakikisha inakuwa na manufaa kwa umma, Mwalimu Nyerere alihakikisha uwekezaji unakuwa wa mfumo maalum wa kitaalamu unaojulikana 'labour Intensive industry'.

Hiyo ina maana ya kuwekeza zaidi katika nguvu kazi kuliko mifumo ya mashine, ili kutanua fursa za ajira, kuliko ya 'capital intensive' inayoegemea zaidi mashine, kuliko nguvu kazi.

Mara moja jiji kama Dar es Saaam kukawekezwa viwanda na kwa namna ya kipekee Barabara ya Pugu (sasa Nyerere) ukawa mtaa wa viwanda bidhaa za nyumbani zikifurika sokoni, Tanzania kuwa nchi ya viwanda na mfumo wa maisha kuwa wa uhuru zaidi.

### MBNEGU AZIMIO ARUSHA

Ni hatua iliyotumika kuimarisha vilivyoamuliwa nchini mwaka 1964, kisiasa na kiutendaji ikiwa ajenda ya kudumu kwa kuhamishia mali zote binafsi kuwa za umma.

Hapo kukaboreshwa kilichoanzishwa na NHC mwaka 1966 katika majengo, safari hii kukizaliwa shirika liitwalo Msajili wa Majumba, inayomiliki majengo yote yaliyotaifishwa. Baada ya miongo kadhaa, asasi hiyo ikaunganishwa na NHC.

Miradi hiyo ikapata ziada ya uwekezaji, pale benki binafsi ya kimataifa iliyotaifishwa kupitia Azimio la Arusha, ikazaa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), mali ya umma.

Hadi unakamilika mpango wa miaka mitano, utumishi wa umma ulishafurika watendaji wenye fani na ndio katika kipindi hicho kukaanzishwa kisheria, Tume ya Rais ya Kusimamia Mashirika ya Umma (SCOPO), ikifafanua tafsiri ya mashirika na utumishi wa umma na maslahi yao.

### DARASA LILILOENDELEA

Tangu kupita Mpango wa Kwanza wa Maendeleo, 1964 - 1969 na wa miaka mitano ulipofuata na baada ya hapo hadi sasa, daima haijawahi kuwa nje ya mikakati kitaifa iliyowekwa na mpango huo.

Mabadiliko yanashuhudiwa tu, kuhusu mahitaji ya wakati kitaifa, mathalan katika mpango wa pili (1969 - 1974) iliendeleza yale yaliyoazimiwa na mpango wa kwanza, kwa sura ya maboresho na mahitaji mapya.

Ndio ikaja suala la kuboresha SCOPO kwa azimio la mwaka 1970, mikutano ya wafanyakazi (sasa sheria) kuanza kujengwa viwanda vya kati vinavyozalisha bidhaa kama majembe, mfano UFI Ubungo na KIZAKU Mbeya.

Pia, kwa viwanda vidogo ili wananchi nao wamiliki; hapo kukaanzishwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mwaka 1973 na mashirika mama kisekta, ya biashara chini ya STC.

Vivyo hivyo, ajenda ya elimu iliimarishwa kwa kofia ya Azimio la Musoma 1974 chini yake ikizaa miradi mingi, miradi ya elimu kupitia UPE; kujua kusoma na kuandika.

Nalo, Azimio la Iringa likaendeleza vijijini vya ujamaa, kuunganisha itikadi ya chama kimoja ya falsafa Ujamaa na Kujitegemea kutoka kilichoamuliwa 1964 na mikakati ya uchumi.

Wahasibu waliosomeshwa Ulaya, miaka ya 1972 wakaanzishiwa chuo IFM, Dar es Salaam, na Bodi yao wahasibu NBAA ikitoa CPA ili wasifuate ACCA, ACA Uingereza na RIA Canada walikoenda wengi.

Kuasisiwa NBC kuliongezewa nguvu katika miaka ya 1970 katika mpango wa pili, Benki ya Nyumba (THB), Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (CRDB) na Benki ya Rasilimali (TIB). Ndiyo zama ambazo reli ya Tazara ilijengwa, kwa mfumo wa 'Standard Gauge' kuanzia mwaka 1975, leo hii inashuhudiwa reli kama hiyo inajengwa itakayotumia umeme.

Hata baada ya kukamilika mpango huo mrefu, ukaibuliwa mwingine wa muda mrefu wa maendeleo ya viwanda wa miaka 20 ukilenga viwanda mama kama vya kuzalisha mashine, kukishuhudiwa kiwanda cha kuunganisha magari Kibaha (TAMCO).

Hata hivyo, mpango huo ulioanza 1976 ulisuasua, kwani Tanzania ilikuwa imetoka kwenye njaa kubwa ya 1974 na miaka michache 1978 ikakutana na vita na Uganda iliyoigharimu, huku mwaka 1985 ukawa mwisho wa mfumo hodhi kisiasa na kiuchumi, Mwalimu Nyerere naye aking'atuka, akiwa na rekodi ya kujenga zaidi ya viwada 410 kwa mujibu wa mtafiti, Dk. Neville Ruben.

Hata hivyo, ikifuatiliwa awamu zote za uongozi nchini zinaendeleza ya miaka mitano, 1964 - 1969, mfano awamu ya pili ilitanua elimu na idadi ya vyuo vikuu nchini, kukishuhudiwa kuanzishwa vyuo vikuu binafsi.


Awamu ya tatu, kukaanzishwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM na kama hiyo kwa sekondari (MMES), huku awamu inayofuata mwaka 2007 kukaanzishwa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

Awamu ya tano, ikarejea zama za 1969 za elimu bure kuanzia msingi hadi kidato cha nne na mapinduzi ya viwanda hadi Tanzania kuingia katika hadhi ya uchumi wa kati, asasi za umma 'SU' zikirejeshwa, ikiwamo benki ya kilimo.

Kwa ujumla, hata mengi yaliyoko sasa, kwa kiasi kikubwa kuanzia na kipengele Ujamaa kwenye katiba, uzalishali hata Muungano wa nchi unaoboreshwa, unarejea makubwa yaliyoamuliwa mwaka 1964.

***• Usikose simulizi zaidi Jumatano ijayo.***

## TAFAKURI YA MLALAHOI




# Bunge mbashara tutarajie mapya?



NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

KUNA nyakati unaweza kukaa ukafikiria mabadiliko ya nchi kisiasa, kijamii na kiuchumi na usipate jibu la kwa nini yanatokea.

Yapo ambayo hutokea kwa sababu za kimazingira, yakihusisha tabianchi, kwa mfano ukame, mafuriko lakini pia vimbunga na tufani, vyote ni kutokana na hali hiyo.

Utabaini yanayotokea kutokana na fikra za watu au hulka tu, kwamba leo unaamua kula maharage na kesho nyama, keshokutwa sukuma wiki na kadhalika.

Au unaamua tu leo unavaa lubega, kesho kimini na keshokutwa ...na maisha yanakwenda. Ni fikra tu na jinsi jamii inavyokutazama. Ukifikiria sana utaumiza kichwa tu.

Lakini, wakati mwingine unaweza kuamua kuonekana hivyo, ukakamatwa kuwa pengine ni muhuni au mzururaji, pia ukakimbizwa hospitalini kwa kudhaniwa chizi, ingawa sivyo.

Mimi hapa nafikiria na kujiuliza, hivi ni kwanini Februari 2016 ikaamuliwa eti kuanzia wakati huo hakuna kurusha matangazo ya televisheni mbashara, tena yaliyohusu mikutano ya Bunge!

Hata wewe hapo ukijiuliza unaweza kuja na majibu kweli? Unaweza kukubali sababu iliyotolewa mwaka ule, eti ni kutokana na gharama za kurusha matangazo hayo?

Matangazo haya yalianza kurushwa miaka nenda rudi, kabla na baada ya televisheni, leo (2016) ghafla eti gharama imekuwa kubwa hivyo tutarekodi na kurusha usiku,tukakubali wana wa Mungu.

Maisha yakaendelea, leo baada ya miaka sita, tunaruhusu matangazo hayo sasa kuwa mubashara, baada ya studio yetu ile ya Bunge kufanyiwa maboresho, sasa mtawasikia mliowachagua.

Hivi kulikuwa na haki gani kutufanyia vile, wakati Bunge ni letu na televisheni ni zetu? Hakukuwa kuoneana kweli?

Sawa, sisi ni wa kukubali, tufanyeje? Lazima tupongeze kwa kutufungulia macho na masikio yetu wenyewe. Haya tumefunguliwa sasa tutayasikia yapi katika Bunge hili la karibia chama kimoja?

Hivi nani ataibuka na kuwa kama wale jamaa zetu chini ya Njelu Kasaka? Wengine, Ndembwela Ngunangwa, Mathias Kihaule, Mussa Nkhangaa, Edward Ayila, Adam Karumbeta, Halimeshi Mayonga, Dk John Katunzi, Ismail Ivwata, Tobi Mweri na Aidan Livigha.

Nao Tabitha Siwale, Obel Mwamfupe, Othman Mpakani, Evarist Mwanansao, Paschal Degera, Erasto Losioki, Nassoro Malocho, Charles Kagonji, Venance Ngula na Benedict Losurutia.

Walikuwapo pia, Deogratias Mwita, Phineas Nnko, John Mwanga, Guntram Itatiro, Paschal Mabiti, Edith Munuo, Raphael Shempemba, John Mhina, George Nhigula, Charles Kinuno, Christian Fundisha, Samuel Ruangisa na Maria Kamm.

Je, katika Bunge hili sasa yetu macho na masikio, tuone na tusikie kinagaubaga nini wanajadili kuhusu maslahi yetu na kama ndicho tulichowatuma.

Hapa lazima kama wanaitaka 2025 waupige mwingi utakaotugusa. Vinginevyo .... Alamsiki!

UCHUMI

# Katambi aibua mpango kuwasuka vijana nchini kumiliki uchumi wao

• Wadau, wafadhili waorodhesha hisia zao ziliko




Naibu Waziri Katambi (wa pili kushoto), alipozindua mradi wa vijana, huku akishuhudiwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wa Ubalozi wa Uswisi nchini, UNFPA na Umoja wa Mataifa. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Sabato Kasika na Yasmine Protace**

JUMATATU wiki hii Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi alizindua mpango wa kuboresha na kuimarisha ustawi na maendeleo ya vijana katika maeneo ya afya, elimu, ushiriki na uwezeshaji kiuchumi, uitwao 'Safeguard Young People Programme.'

Mikoa inayonufaika kwa sasa ni Kigoma, Shinyanga, Simiyu, Dar es Salaam, Dodoma, Zanzibar na Pemba, ikilenga kuwapa elimu vijana wajitambue na washiriki katika utungaji sera na mikakati yote nchini, inayohusu kuongeza uwezo na kupanga sera rafiki kwao.

Pia, unalenga kuongeza ushiriki wa vijana katika kamati za maendeleo za maeneo yao, kuwaongezea uelewa wa elimu ya afya ya uzazi na ujuzi wa maendeleo yao.

Naibu Waziri huyo anasema katika masuala yanayohusu ustawi wa vijana, serikali inazingatia zaidi afya yao, kuhakikisha uchumi unaimarika na furaha yao inadumu. Mpango unaendana na kipaumbele kwao na kuwajengea uwezo.

**NAFASI YAO VIJANA**

Naibu Waziri huyo anasema, duniani vijana ndio wanaochangia kwa kiasi kikubwa kukuza na kujenga uchumi wa mataifa yao, kwani ndio nguvukazi ya taifa.

“ Hapa nchini, matokeo ya utafiti wa nguvukazi ya taifa wa mwaka 2020/21 unaonyesha idadi ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 inakadiriwa kufikia watu milioni 18.3,” anasema.

> **“Mwishoni tunataka kuona vijana wanahusika katika utungaji wa sera na mikakati yote ya nchi inayowahusu, kuongeza uwezo na uchechemuzi wa kupanga sera rafiki kwa vijana.**

Anasema inajenga tafsiri kiwango chao kushiriki katika shughuli za kiuchumi na za kijamii kwa ujenzi wa taifa kipo wastani wa asilimia 80. Lakini bado wanakabiliwa na vikwazo kama ajira, kukosa usawa wa kuzifikia fursa muhimu, afya ya uzazi, ukatili wa kijinsia na ujuzi.

“Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kushughulikia vikwazo vyao na utekelezaji wa programu ya stadi za maisha ikijumuisha elimu ya kujitambua, uthubutu, kuweka malengo na kufanya maamuzi sahihi,” anasema.

Anafafanua kuwa serikali inaendelea kutekeleza programu ya ukuzaji na kurasimisha ujuzi nchini, kuwaongezea ujuzi vijana, waajiriwe na kujiajiri.

**VITA VYA UKATILI**

Katambi anasema, serikali inaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWA), kuhakikisha taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia vinashughulikiwa kwa wakati na kwa kufuata utaratibu unaofaa.

“Serikali pia inasimamia utekelezaji wa ajenda ya kitaifa ya kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana (NAIA). Ajenda hii ya kitaifa ilizinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Aprili 17 mwaka jana,” anasema.

Anataja vipaumbele vyake ni kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kutokomeza mimba za utotoni, kuondoa ukatili ikiwamo ukatili wa kingono, kimwili na kisaikolojia.

“Vipaumbele vingine ni kuboresha hali ya lishe, kuhakikisha watoto wa kike na kiume wanabaki shuleni na kuwajengea vijana ujuzi na uwezo wa kuzifikia fursa mbalimbali za kiuchumi,” anasema.

Anatoa rai kwa sekta zote na wadau wanaotekeleza mpango huo, kuhakikisha unaendana na malengo ya ajenda ya kitaifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo kwa vijana.

“Ikumbukwe kuwa unaendana na malengo ya Dira 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Malengo ya Maendeleo Endelevu na Makubaliano ya Mawaziri wenye dhamana ya Vijana.

“Elimu na Afya kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESA Commitment) kuhusu kuwekeza katika maendeleo ya vijana ili kuwa na vijana wenye afya bora, walioelimika, na wanaowajibika katika nchi zao,”

**WADAU WAORODHESHA**

Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini, Zlatan Milisic, anasema bila vijana hakuna maendeleo ya nchi, muungano wa pamoja katika jamii, na wala hakuna maendeleo ya nchi.

Anataja ni muhimu vijana waandaliwe kwa maendeleo yao na taifa, kwa kuwezeshwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo kuelimishwa wajitambue na kusimamia haki zao.

Mark Bryan Schreiner, Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, anasema mpango huo wa kimaendeleo tangu mwaka 2013, Uswisi iliunga mkono Ofisi ya Kanda ya kusini mwa Afrika ya UNFPA kwa kuuzindua katika nchi nane za Zimbabwe, Eswatin, Malawi, Zambia, Afrika Kusini, Botswana na Lesotho.

Mwakilishi Mkazi huyo anataja nyingine ambazo mpango huo umefika kuwa ni Rwanda, Msumbiji na sasa umezinduliwa rasmi Tanzania.

Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot anasema kupitia mpango huo kwa vijana, ubalozi unategemea kushiriki kikamilifu kuhakikisha vijana wanapata nguvu ya pamoja katika kuhusishwa kwenye maamuzi yote ya vijana.

Anasema kundi hilo linatakiwa kuepushwa na maambukizi mapya ya VVU, mimba zisizotarajiwa, ndoa za utotoni ikiwamo aina zote za ukatili ili waweze kupaza sauti zao na kutetea mabadiliko.

“Tuwafikirie vijana kama viongozi wa sasa wanaoweza kuendesha uvumbuzi na ukuaji wa uchumi. Huu ndio mustakabali ambao Uswisi UNFPA na serikali ya Tanzania wanaufikiria,” anasema.

**MILIONI 57 KUFIKIWA**

Ofisa Vijana wa UNFPA, Fatina Kiluvia, anasema mpango huo unalenga vijana ambao ni kundi kubwa walio katika balehe kuanzia miaka 10 hadi 24 na kwamba ndio wanakumbwa na vikwazo vingi.

“Vijana balehe, zaidi ya milioni 57 nchini, ndio wanatarajia kunufaika kwa sababu wao ndio waathirika wakuu wa matatizo yanayohusu vijana, wao ndio wanakumbwa na ndoa za utotoni, mimba za utotoni, wanaacha shule kusaidia familia kiuchumi, wanatoroka majumbani wakiona hawaelewi mazingira na huko waendako wanakutana na dunia katili zaidi,” anasema Fatina.

Katika kutekeleza mpango huo, zimetangwa Dola milioni 5.1 za Kimarekani na kwamba SYP inawahusu vijana kama kundi la kwanza, pia itawagusa wadau wote wanaohusika na vijana kama wazazi, viongozi wa dini, watunga sera, na viongozi wa mitaa na vijiji ambao ndio wakuu wa maeneo husika.

“Mwishoni tunataka kuona vijana wanahusika katika utungaji wa sera na mikakati yote ya nchi inayowahusu, kuongeza uwezo na uchechemuzi wa kupanga sera rafiki kwa vijana,” anasema.





## Sekretarieti ya Ajira yaongezewa bajeti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeongeza bajeti Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kutoka Sh. bilioni 3.3 kwa mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 8.7 kwa mwaka ujao wa fedha 2022/23 ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Katibu Mkuu wa Sekretarieti hiyo, Mhandisi Samwel Tanguye, aliyasema hayo jana alipokuwa akitaja mafanikio yaliyopatikana ya ofisi hiyo katika mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema pia Ofisi hiyo wameongezewa Sh. milioni 689 nje ya bajeti iliyoidhinishwa mwaka jana na hivyo kufanikisha kutekeleza majukumu yao kirahisi katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tunamshukuru sana Rais kutokana na kuijali taasisi hii, Sekretarieti ya Ajira itaendelea kutekeleza jukumu la kuendesha mchakato wa Ajira kwa kuzingatia sheria,kanuni na taratibu ikiwamo miongozo mbalimbali kwa weledi," alisema.

Alisema Sekretarieti inaendesha shughuli zake kwa kufuata taratibu, sheria na kanuni kwa kushirikiana na Wizara na Mamlaka za Serikali ili upatikanaji wa watumishi wa umma wenye vigezo. Pamoja na hayo, alisema ndani ya mwaka huo mmoja wa Rais Samia wametoa vibali vya ajira 2,876 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Uhandisi.

"Kwa TRA vimetolewa vibali vya ajira 2100, TRC vimetolewa vibali 508 na upande wa Uhandisi vibali vya ajira vilivyotoka ni 268, ni rekodi ya aina yake kutolewa kwa wananchi ndani ya mwaka mmoja wa utendaji kazi wa Rais Samia," alisema.

Alihimiza jamii kutumia mfumo wa kidigitali wa Ajira (Ajira Portal Mobile App) kuomba nafasi za kazi zinazotangazwa, kwa kuwa mfumo huo haudanganyi bali unatoa taarifa sahihi juu ya uwapo wa nafasi hizo kupitia simu ya kiganjani.

# Wathamini sasa wapewa siri ya kutocheleweshea wananchi fidia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amewataka wathamini kufanya kazi kwa kuzingatia maadili, sheria na miongozo ili kuondokana na kero za ucheleweshaji fidia kwa wananchi. Silinde alitoa maelekezo hayo katika mahafali ya kwanza ya usajili wa kudumu wa wathamini yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema kumekuwapo na baadhi ya wathamini wanaofanya kazi kwa kutozingatia miongozo na kusababisha wananchi kucheleweshewa fidia.

"Taaluma hii bado inakabiliwa na changamoto za kiutendaji, kwa baadhi ya wathamini na tunaomba Bodi yako Mwenyekiti izifanyie kazi nawasihi mkatende haki na uaminifu kwa kila mtakayemhudumia,"alisema.

Aliwataka katika utekelezaji wa majukumu yao kuzingatia kiapo ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mthamini Mkuu nchini, Evelyne Mgasha, alisema ofisi yake itaendelea kutoa miongozo kwa wathamini ili kufanya kazi kwa viwango bora.

"Ofisi ya Mthamini Mkuu itaendelea kushirikiana na Bodi ya usajili wa wathamini katika kuhakikisha inasimamia vyema kazi za uthamini na kuendeleza kutoa miongozo katika matumizi ya viwango vya uthamini,"alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wathamini nchini, Dk.Cletus Njovu, alisema tangu kuundwa kwa bodi hiyo imefanikiwa kutatua kero kadhaa za ucheleweshaji wa fidia kwa wananchi.

"Bodi ilifanikiwa kusimamia nidhamu kati ya wathamini waliosajiliwa pamoja na kampuni ambapo hatua mbalimbali za kinidhamu zimechukuliwa na zinaendelea kuchukuliwa kwa watu binafsi walioshirikiana kufanya kazi mbalimbali ambazo hazikidhi viwango, weledi na haki, pamoja na kampuni zote zinazohusika na makando kando hayo,"alisema.

Alisema Bodi imepokea kesi za kinidhamu zaidi ya 20 ambapo kati ya hizo kuna kampuni nne zimetozwa faini, kampuni tatu zimepewa onyo kali kuhusu tabia zao, na wakirudia kosa watapewa adhabu kali zaidi ikiwamo kuwafutia usajili.




Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru (wa pili kushoto), akikabidhiwa kibao cha anwani ya makazi na Mratibu wa mradi huo jijini humo, Joseph Nkuba, kwa ajili ya kukiweka katika Mtaa wa CDA, ilipo ofisi ya Jiji hilo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Elimu kuhusu soko la pamoja EAC kutolewa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kuhamasisha wananchi wa Afrika Mashariki kuzichangamkia fursa zinazotokana na mtangamano wa Jumuiya, Bunge la Afrika Mashariki limeandaa mpango wa kutoa elimu kwa umma kushiriki kwenye utekelezaji wa hatua za soko la pamoja.

Mwenyekiti wa Wabunge wa Tanzania wa Bunge hilo, Adam Kimbisa, ndiye aliyezungumzia hatua hiyo jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Kimbisa alisema lengo kubwa ni kuhamasisha wadau washiriki kwenye utekelezaji wa hatua ya soko la pamoja la Afrika Mashariki.

"Mpango huu unatekelezwa katika nchi zote wanachama na umeanza Aprili 3 hadi 8 mwaka huu,"alisema Kimbisa.

Alisema kwa upande wa Tanzania mpango huo unatekelezwa na wabunge wa Tanzania wa Bunge hilo kwenye Jiji la Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

"Shughuli zinazofanyika ni pamoja na kuonana na watendaji wa Wizara mbalimbali ili kuona utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa kuhusu soko la pamoja, kukutana na waandishi wa habari, kushiriki vipindi vya redio na televisheni na kuonana na wadau mbalimbali."

"Kama mnavyofahamu Jumuiya ya Afrika Mashariki ilirejeshwa rasmi mwaka 1999 na nchi za Tanzania,Kenya na Uganda, mwaka 2007 ziliongezeka nchi za Burundi na Rwanda,"alisema.

Alisema mwaka 2016 Jamhuri ya Sudani Kusini nayo ilijiunga na jumuiya na mwaka huu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imeingia rasmi.

"Ni ukweli usiopingika kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwa kivutio kwa wengi ndiyo maana nchi nyingi zimeendelea kujiunga nayo.Fursa zilizopo katika Jumuiya ndiyo kivutio na sababu ya msingi inayozisukuma nchi mbalimbali kuendelea kujiunga,"alisisitiza Kimbisa.

Aidha, alisema kulingana na Mkataba, mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unatekelezwa kwa hatua nne.

Alisema hatua hizo ni umoja wa Forodha, Soko la pamoja ,Umoja wa Fedha na Shirikisho la Kisiasa.

Vilevile, alisema mkataba umeainisha maeneo ya ushirikiano katika sekta mbalimbali ikiwemo biashara, uwekezaji maendeleo ya viwanda,sekta ya fedha,miundombinu,sayansi na teknolojia ,kilimo na chakula ,mazingira na maliasili, utalii na wanyama pori ,siasa ulinzi na usalama pamoja na sheria na mahakama.

"Hatua ya tatu katika mtangamano wa Afrika Mashariki ni Umoja wa Fedha katika hatua hii nchi wanachama zimekubaliana kuwa na sera moja ya fedha na kutumia sarafu moja katika nchi zote wanachama,"alisema Kimbisa.

Kadhalika, alisema hatua hiyo ni muhimu katika kurahisisha biashara na maisha kwa ujumla kwani itawawezesha kuondokana na utaratibu wa kubadilisha fedha kila unapovuka mipaka kutoka nchi moja kwenda nyingine.

"Majadiliano ya itifaki ya umoja wa Fedha yalikamilika mwaka 2013 ambapo nchi wanachama zilikubaliana kuwa na kipindi cha maandalizi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2014 mpaka mwaka 2024,"alisema Kimbisa.

Pia, alisema Bunge la Afrika Mahariki limetunga sheria mbili za kuanzisha taasisi za jumuiya zitakazo simamia mchakato wa Umoja wa Fedha na pia linaendelea na miswada mingine inayolenga kuanzisha taasisi zitakazo tekeleza makubaliano hayo.

Naye, Mbunge wa Bunge hilo, Maryam Ussi Yahaya, alisema baada ya DRC kujiunga na Jumuiya hiyo hivi sasa soko la pamoja lina jumla ya watu milioni 271 ambao Tanzania inapaswa kuwatumia kama fursa ya kufanya biashara katika nchi wanachama.



# Bil. 1.34/- zakarabati shule Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KATIKA kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, mkoa wa Mbeya umepokea zaidi ya Sh. bilioni 1.34 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 636 katika shule mbalimbali za msingi na sekondari.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano maalumu wa kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye mkoa katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia.

Mkutano huo ulishirikisha taasisi mbalimbali za umma za mkoa wa Mbeya pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo na kudhaminiwa na Shule ya Paradise Mission iliyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani hapa.

Homera alisema kati ya madarasa hayo yaliyojengwa, 464 yamejengwa kwenye shule za sekondari na 172 yamejengwa kwenye vituo mbalimbali shikizi hasa kwenye maeneo ya vijijini ili kurahisisha upatikanaji wa elimu.

Alisema mbali na miradi hiyo ya vyumba vya madarasa, pia imetekelezwa miradi ya ukarabati wa shule kongwe za sekondari ndani ya mkoa ikiwamo Shule ya Sekondari Rungwe ambayo imekarabatiwa kwa zaidi ya Sh. milioni 752.

Alisema kwenye ukarabati wa shule hiyo miundombinu iliyoboreshwa ni vyumba vya madarasa, ofisi za walimu, vyoo na mabweni ya kulala wanafunzi.

"Lakini pia katika kipindi hicho, mkoa wetu ulipokea zaidi ya Sh. milioni 11.5 kwa ajili ya kugharimia elimu bila malipo, Sh. bilioni 4.7 ni kwa ajili ya shule za msingi na Sh. bilioni 6.8 kwa shule za sekondari," alisema Homera.

Homera alisema katika kipindi hicho, serikali imeboresha miradi mbalimbali ya uboreshaji wa miundombinu kwenye vyuo mbalimbali katika mkoa huo vikiwamo vyuo vikuu na vyuo vya kati.

Katibu Tawala wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema mbali na uboreshaji wa miundombinu ya elimu, sekta zingine pia zimenufaika kwa kupatiwa fedha za utekelezaji wa miradi zikiwamo kilimo, afya na barabara.

Alisema katika kipindi hicho, mkoa ulipokea Sh. bilioni 20.3 kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya, Sh. bilioni 19.5 miradi ya maji, Sh. bilioni 41.7 miundombinu na Sh. bilioni 4.1 kwa ajili ya nishati.

Baadhi ya wadau walioshiriki mkutano huo kutoka sekta binafsi, walisema pia wamenufaika kutokana na utekelezaji wa miradi uliofanywa na Serikali katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani.

Mmoja wa wadau hao, Ndele Mwaselela ambaye ni mmiliki wa Shule za Patrick Mission za mkoani Dar es salaam na Paradise Mission ya Mbeya, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja, wawekezaji wamekuwa na mazingira rafiki ya kufanya shughuli zao.

Alisema kwa kawaida mfumo wa uwekezaji hasa kwa wadau wa sekta binafsi na wafanyabiashara huwa unategemea zaidi busara za kiongozi wa nchi.

Mwaselela alisema wawekezaji wanafanya kazi kwa amani kutokana na mfumo wa ukusanyaji wa kodi kuwa rafiki zaidi kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo wawekezaji walikuwa wanafungiwa akaunti zao na kwamba baadhi ya maofisa wa TRA walikuwa wanatumia mabavu kukusanya kodi.



Baadhi ya wadau wa maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, wakifuatilia hotuba ya Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera (hayupo pichani), kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, kwenye mkutano uliofanyika juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mchungaji KKKT adai kutishiwa usalama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, umeendelea kuwaweka njiapanda baadhi ya wachungaji katika usharika huku wengine wakipokea vitisho kutoka kwa waumini na kutakiwa waondoke.

Mchungaji wa Usharika wa Isanga jijini Mbeya, Nelson Mlungu, ni mmoja wa wachungaji waliopata vitisho huku akidai kuwa amekuwa akitishiwa usalama wake kutoka kwa waumini hasa vijana.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mchungaji Mlungu alisema vitisho ambavyo amekuwa akipokea kutoka kwa waumini vimekuwa vikiivuruga familia yake na kwamba kwa sasa yuko njiapanda na hajui hatima yake.

Alisema kitisho kikubwa alichokipata hivi karibuni ni kwamba vijana walimpatia saa 24 asionekane usharikani hapo hali ambayo alisema ilimvuruga zaidi lakini hakuondoka kwa sababu alikuwa anasubiri uamuzi wa Baraza la Wazee la Usharika huo.

"Aliyeniambia alisema amekuja kuleta ujumbe kwa niaba ya wakristo wote. Ujumbe huo kwa kweli ulinifedhehesha sana, nilijiona niko peke yangu lakini nilipopigiwa simu na wazee kwamba kuna jambo wanataka kuongea nami nikafarijika kidogo," alisema Mlungu. Aliwaomba viongozi wote wanaohusika kwenye mgogoro ndani ya dayosisi kurudi mezani na kuutatua kuliko hali iliyopo kuendelea ambayo alisema inavuruga sifa ya kanisa.

Baadhi ya wazee wa kanisa katika usharika huo, walisema matamko yanayotolewa na vijana wa kanisa hilo dhidi ya mchungaji, hawayaungi mkono na yanawakera, hivyo wakamtaka mchungaji huyo kuendelea kuwa na mania wakidai wataendelea kumhudumia.

Mmoja wa wazee hao, Jackson Mwakasisi, alisema vijana walianza kuleta vurugu kanisani hapo kwenye ibada ya Jumapili kwa kurushiana maneno na mchungaji katikati ya ibada ambayo alisema yaliwakera wazee.

Alisema wazee hawaungi mkono mchungaji wao kuondoka kwa kuwa amewaletea maendeleo kwenye usharika katika kipindi ambacho amehudumu mahali hapo.

Mwakasisi alisema vitendo vilivyofanywa na vijana vinaashiria kutaka kumdhalilisha mchungaji huyo, hivyo wamekubaliana kuhakikisha wanamlinda katika kipindi chote cha mgogoro unaoendelea.

Naye Tumpe Njaku alisema kitendo cha vijana kutaka kumfukuza mchungaji huyo ni kutaka kuvuruga amani ya kanisa, hivyo akawataka kuacha mambo hayo na kwamba wao wataendelea kumheshimu.

Alisema wazee hawaoni kosa lolote la mchungaji na kwamba endapo angekuwa na makosa, vijana walitakiwa kuwasilisha kwenye baraza la wazee ili wasuluhishe lakini si kuanza kumtishia.

Njaku alisema hawajaona kosa lolote la mchungaji huyo, hivyo hawataruhusu aondoke kwa namna yoyote.

Mwishoni mwa wiki, vijana wa usharika huo hilo walisema hawamtaki mchungaji huyo kwa sababu anamuunga mkono aliyekuwa Askofu wa Dayosisi ya Konde, Dk. Edward Mwaikali, ambaye aliondolewa madarakani na Mkutano Mkuu wa Dayosisi.

Vijana hao pia walisema wanasitisha kupeleka asilimia ya sadaka zao kwenda kwenye Dayosisi na KKKT Makao makuu kwa ajili ya kuhudumia maeneo hayo.

## Wakamatwa madai ya kukutwa ya bangi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeanzisha oparesheni maalumu la kuwasaka na kuwasweka ndani vijana wote wanaofanya biashara ya dawa za kulevya aina ya bangi pamoja na watumiaji wa bidhaa hiyo haramu.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema jana kuwa katika oparesheni hiyo wameshakamata watu watatu ambao wanauza na kusafirisha dawa hizo haramu ndani ya mkoa.

Matei alisema katika tukio la kwanza, makachero wa jeshi hilo walimkamata Emmanuel Andrew (48 ) mkazi wa Inyala katika Kata ya Iyunga jijini Mbeya akiwa na kete 16 za bangi ambazo ni sawa na gramu nane.

Alisema mtuhumiwa ni mfanyabiashara na mtumiaji wa bangi, hivyo wanaendelea na uchunguzi ili kubaini wenzake ambao anashirikiana nao kwenye biashara hiyo.

Katika tukio lingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linamshikilia Salum Karibu (30) mkazi wa Makongolosi wilayani Chunya ambaye ni dereva akiwa anasafirisha bangi kwenye gari akiwa amezihifadhi katika boksi.

Alisema kijana huyo alikutwa anasafirisha kete 132 sawa na gramu 800 za dawa hizo kwenye gari aina Mitsubish Fuso lenye namba za usajili T.206 DPP.

Katika tukio la tatu, Kamanda Matei alisema polisi wanamshikilia Andrew Essabitory (25) mkazi wa ZZK katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani hapa kwa tuhuma za kukutwa na gramu 400 za bangi na kwamba alikuwa anauza kete mbili kwa Sh. 500.

Alisema uchunguzi wa matukio yote unaendelea na kwamba uchunguzi huo ukikamilika wahusika watafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.







Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (wa tatu kushoto), akizungumza alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Samia kuzindua nembo ya sensa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kuzindua nembo ya sensa ya watu na makazi Mjini Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera , Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Hamza Hassan Juma, alisema maandalizi ya uzinduzi huo yamekamilika.

Alisema sensa ya mwaka huu ni sensa ya sita kufanyika Tanzania ambapo hufanyika kila baada ya miaka 10 ambapo kwa mara ya mwisho ilifanyika mwaka 2012.

Hamza alisema kuwa madhumuni ya sensa ya watu ni kusaidia upatikanaji wa takwimu sahihi zilizochambuliwa ili kuandaa na kutekeleza sera, kufuatilia na kutathmini mipango na programu za maendeleo katika ngazi ya kitaifa ,kikanda na kimataifa .

Alieleza kuwa sensa hutoa takwimu sahihi zitakazowezesha serikali kupanga usahihi mipango ya maendeleo kwa ajili ya watu wake katika nyanja zote za mahitaji ya msingi .

Alisema nembo ya sensa inayobeba kauli mbiu ya pamoja na tarehe ya sensa katika hatua za awali za uhamasishaji ni muhimu kwa kuwa ni nyenzo ambayo inatambulisha sensa katika namna ambayo ni rahisi na shirikishi.

Aliwataka wananchi kijitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuhesabiwa kuiwezesha serikali kupanga mipango yake ya maendeleo kwa sababu bila ya kuwa na takwimu sahihi, serikali itashindwa kupanga mipango yake ya maendeleo kama ilivyokusudiwa .

Naye Kamishna wa sensa kwa upande wa Zanzibar, Balozi Mohammed Hamza, alisema wamejipanga ili kuhakikisha kuwa sensa ya mwaka huu inakamilika kama inavyotarajiwa kufanyika .

Alifahamisha kuwa wamejipanga kutoa elimu kwa jamii ili wananchi wote wajue umuhimu wake.

# Mwinyi akoshwa CBE kujenga kampasi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekipongeza Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa kujenga kampasi yake Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi alitoa pongezi hizo Ikulu Zanzibar alipofanya mazungumzo na uongozi wa Chuo hicho ulioongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Wineaster Sania Anderson.

Dk. Mwinyi aliueleza uongozi huo kwamba uamuzi wa kujenga kampasi Zanzibar utawasaidia kwa kiasi kikubwa wanafunzi wa Zanzibar ambao walikuwa wakifuata elimu ya biashara Tanzania Bara.

Alisema Serikali ya Zanzibar iko tayari kutoa ushirikiano katika kuhakikisha chuo hicho kinajenga kampasi yake na uwamuzi huo ni mzuri na unahitaji ushirikiano.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alipongeza azma ya chuo hicho ya kutoa mafunzo kwa vijana walioishia kidato cha pili ambao wameshindwa kuendelea na elimu ya juu.

Aliongeza kuwa hatua ya kuwasomesha vijana walioishia kidato cha pili na kushindwa kuendelea na elimu ya juu ni miongoni mwa malengo na mikakati iliyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alieleza kwamba Serikali ya Zanzibar inaendeleza mikakati yake ya kuimarisha elimu ya vyuo vya amali ili kuhakikisha vijana walioshindwa kuendelea na elimu ya juu nao wanapata elimu za stadi za maisha katika vyuo hivyo Zanzibar.

Naye Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Anderson alisema mchakato wa kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho umeshafanyika na kupongeza ushirikiano mzuri walioupata kutoka Serikali ya Zanzibar.

Alieleza hatua zitakazochukuliwa na uongozi huo kupitia Serikali ya Tanzania katika bajeti yake juu ya utaratibu wa kuanza ujenzi huo, ambao utakuwa kwa awamu tatu na kutarajiwa kugharimu Sh. bilioni 10.12.

Aidha, alieleza kuwa miongoni mwa wanafunzi watakaowachukua kwa ajili ya kujiunga na chuo hicho kitakapokuwa tayari kuanza mafunzo ni wale walioishia kidato cha pili na kushindwa kuendelea na elimu ya juu ambao watawaanzishia elimu ya cheti mpaka shahada katika kada ya elimu ya biashara.

# Mjini Magharibi kutenga maeneo ujenzi madarasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameuagiza uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi kuhakikisha wanatenga maeneo kwa ujenzi wa madarasa 36 ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

Alitoa maelekezo hayo katika mwendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi inayoendelea kujengwa kwa fedha za ahueni ya UVIKO- 19 katika Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema Serikali imeelekeza kujengwa madarasa 84 katika Wilaya hiyo na kueleza kuwa ni jukumu la Serikali ya Mkoa kuhakikisha wanasimamia upatikanaji wa maeneo ya kujenga na kuwakabidhi makandarasi ambao ni Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) kuanza kazi ndani ya siku kumi.

Hemed alieleza kuwa kukamilika kwa madarasa hayo kutawasaidia walimu kufundisha katika mazingira mazuri na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa Zanzibar.

Aidha aliipongeza JKU kwa hatua nzuri waliyofikia katika ujenzi wa madarasa hayo na kuwasihi kusimamia mkataba ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa.

Kuhusu Hospitali ya Wilaya ya Magharibi 'A' inayojengwa eneo la Mbuzini, Hemed alieleza kuwa kukamilika kwa hospitali hiyo kutapunguza mrundikano wa wagonjwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na itakuwa na vifaa vya kisasi na huduma zote za msingi zitapatikana.

Naye Mkuu wa Wilaya Magharibi 'A' Unguja, Suzan Peter Kunambi, alieleza kuwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ni kilio cha muda mrefu cha wananchi, hivyo inatarajiwa kuhudumia wananchi wa shehia 31 za wilaya hiyo na zingine.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kihinani, Mwanajuma Makame Issa, alieleza kuwa ujenzi wa madarasa katika wilaya hiyo utapunguza masafa kwa Wanafunzi kufuata elimu masafa ya mbali na kueleza kuwa hatua hiyo itapelekea kupunguza vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ENCHANTING TANZANIA SAFARIS LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye namba za usajili T960 DCB, CHASSIS NAMBA JTERB71J900038937, ENGINE NAMBA 1N20544699. Kwa yeyote ataeiona atoe taarifa kituo chochote cha **polisi.POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/139673/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JEROME TITTO KILAWE** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili T 633 AYT – TOYOTA LANDCRUIESER. Chassis namba JTERB71J800049412. Engine namba IHZ0501190. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/139702/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARTHA YONAH JOSEPH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0214.0056** kilichotolewea na Baraza la Mitihani kupitia **MSALATO SEKONDARI** mwaka **2012**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: NJO/NJO/RB/136039/2022.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 38 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE STEPHANO NKOSWE CHUNDU OF MAJENGO WITHIN DODOMA REGION AND IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY STEPHANO ULIZA PIGAUZI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th Day of April, 2022.
Dated at Dodoma this 18th day of March, 2022

..................................................
**PETITIONER**
**Presented for filling this 18th day of March, 2022**

..................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

RESIDENT MAGISTRATE

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:



Wanawake wakipita mbele ya hoteli iliyoharibiwa na mabomu mjini Chernihiv nchini Ukraine, juzi. **PICHA: AP**

# Russia inavyotengwa na G7

**Kyiv,** UKRAINE

KUNDI la G7 la mataifa yaliyoendelea kiviwanda, limesema ni wakati sasa kwa nchi ya Russia, kusimamishwa kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, kwa sababu ya vitendo vyake dhidi ya Ukraine.

Kundi la G7 linajumuisha Canada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Japan, Uingereza na Marekani.

"Picha za kutisha za vifo vya raia, mateso, pamoja na ripoti za unyanyasaji wa kijinsia na uharibifu wa miundombinu ya kiraia zinaonyesha sura halisi ya vita vya kikatili, Russia dhidi ya Ukraine na watu wake," mawaziri wa mambo ya nje wa kundi hilo wamesema kwenye taarifa ya pamoja.

Kauli ya kundi hilo, imekuja kabla ya kura iliyopangwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa iliyotarajiwa kufanyika jana, kuhusu iwapo itaisimamishwa Russia katika Baraza la Haki za Kibinadamu la UN.

Hatua hiyo ilianzishwa na Marekani baada ya kugundulika kwa mamia ya miili baada ya Russia kuondoa wanajeshi wake kwenye miji iliyo karibu na mji mkuu wa Ukraine, Kyiv.

Msemaji wa Baraza Kuu la Umoja huo, Paulina Kubiak amesema kwamba kikao hicho cha dharura cha baraza kuhusu Ukraine kilikutana jana wakati azimio la kusimamisha uanachama wa Russia litakapopigiwa kura. Balozi wa Marekani kwenye Umoja huo, Linda Thomas-Greenfield amesema kwamba wanaamini wanajeshi wa Russia walifanya uhalifu wa kivita nchini Ukraine na kwamba inatakiwa kuwajibishwa.

**Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alihutubia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wiki hii, akisema Russia iwajibishwe, hata hivyo Russia inakanusha kuhusika katika mauaji hayo.**

Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine, anasema Kyiv inalenga kuwahamisha raia kutoka mikoa kadhaa ya Kusini na Mashariki mwa nchi hiyo, kupitia njia 10 za kibinadamu, jana, baada ya kukubaliana na Russia.

Iryna Vereshchuk, amesema katika chapisho kwenye Telegram kwamba raia kutoka mikoa ya Donetsk, Luhansk na Zaporizhzhia watahamishwa hadi miji ya Zaporizhzhia na Bakhmut.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, imesema vikosi vyake viliharibu vituo vinne vya kuhifadhi mafuta katika miji ya Ukraine ya Mykolayiv, Kharkiv, Zaporizhzhia na Chuhuiv usiku kucha.

Mashariki mwa Ukraine sasa inalengwa na mashambulizi ya Kremlin. Raia wametakiwa kukimbia mapigano yanayojiri, licha ya vikwazo vipya vya Marekani dhidi ya Russia.

Jumatano wiki hii, Kyiv ilitoa wito kwa raia wake kuondoka Mashariki mwa nchi kutokana na tishio la mashambulizi ya Russia.

Mjini Mariupol takriban watu 100,000 wanasubiri eneo la bandarini, ili kuondolewa.

Severodonetsk, jiji la Mashariki linalodhibitiwa na jeshi la Ukraine, ndilo lililolengwa na mashambulizi.

Marekani ilitangaza kuziwekea vikwazo benki kubwa za Russia, Sberbank na Alfa Bank na binti wawili wa Rais Vladimir Putin baada ya ugunduzi wa miili mingi ya raia katika miji kadhaa karibu na Kyiv.

Umoja wa Ulaya (EU), bado uko kwenye majadiliano ya kuamua hatua mpya ya vikwazo, inayolenga hasa sekta ya nishati.

Katika eneo la Kyiv, ambalo jeshi la Russia, limeondoka, hofu ya ugunduzi mpya wa miili ya watu waliouawa inaongezeka baada ya mauaji ya Bucha.

Ripoti mpya zimebaini kwamba maeneo kadhaa ya Ukraine yamekumbwa na matukio mabaya zaidi.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky alihutubia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wiki hii, akisema Russia iwajibishwe, hata hivyo Russia inakanusha kuhusika katika mauaji hayo.

Nchi ya Hungary, jana ilipokea shehena ya kwanza ya mafuta ya nyuklia kwa ajili ya kinu chake cha Paks .

Shehena hiyo kutoka Russia ilifika nchini humo kwa njia ya anga juzi, baada ya mashambulizi kati ya Russia na Ukraine kuanza, usafirishaji wa meli kwa njia ya reli kutowezekana,

Waziri wa Mambo ya Nje Hungary, Peter Szijjarto amesema kuwa nchi yake ilikataa vikwazo vyovyote kwa mafuta na gesi dhidi ya Russia na kuongeza kuwa kuweka vikwazo vyovyote katika shughuli zinazohusiana na nishati ya nyuklia pia ni hali ya hatari kwa Hungary.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov amesema Kyiv imewasilisha Moscow rasimu ya makubaliano ya amani lakini ina masuala ambayo hayakubaliki.

Amesema Ukraine ilirekebisha mapendekezo yake ya awali yaliyotolewa wakati wa mazungumzo kati ya Russia na Ukraine, mjini Istanbul Machi 29, mwaka huu.

Lavrov anadai Kyiv inadhibitiwa na kituo cha serikali cha Marekani mjini Washington ambao wanamsukuma Rais Volodymyr Zelensky kuendeleza uhasama. Amesema Russia itaendelea na mazungumzo, ingawa itasimamia madai yake katika makubaliano yoyote.

Ukraine imejibu kwamba, maoni ya Lavrov ni propaganda, na hahusiki moja kwa moja katika mazungumzo akisema yanapaswa kuonekana katika mwanga na umakini kutokana na matukio ya mji wa Bucha.

• ***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

# MTANZANIA KUCHEZESHA ROBO CAF MAMELODI NA ATLETICO

**Na Adam Fungamwango**

MWAMUZI wa Tanzania, Frank Komba ameendelea kufanya vema kwa kuipeperusha vizuri bendera ya nchi baada ya kuchaguliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuchezesha mechi ya robo fainali Ligi ya Mabingwa kati ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini na Atlético Petróleos de Luanda ya Angola.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka nchini Tanzania (TFF), imesema kuwa Komba ameteuliwa kuwa miongoni mwa waamuzi watakaochezesha mchezo huo wa robo fainali ya pili, Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya timu hizo, utakaochezwa kwenye Uwanja wa FNB, Johannesburg, Afrika Kusini Aprili 23, mwaka huu.

Mechi ya kwanza ya robo fainali hiyo inatarajiwa kuchezwa Uwanja wa 11 de Novembro nchini Angola, Aprili 16, mwaka huu ambapo Atletico Petroleos itakuwa nyumbani dhidi ya majirani zao hao kutoka Afrika Kusini.

Komba, ambaye ni mshika kibendera, amekuwa ni mwamuzi anayeiwakilisha vema nchi, akichaguliwa na CAF, kuchezesha mechi mbalimbali kubwa, ambapo hivi karibuni alikuwa mmoja wa waliochezesha fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) nchini Cameroon.

Mwamuzi huyo anakwenda Sauzi ambako pia timu ya Tanzania, Simba inatarajiwa kwenda kucheza mechi ya pili ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Afrika, dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini utakaochezwa Aprili 24, mwaka huu baada ya ule ya awali ambao unatarajiwa kuchezwa Aprili 17 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**TUMEICHUKUA...**




Baadhi ya wachezaji, mashabiki na viongozi wa timu ya Kijiwe Nongwa FC ya Muheza, Tanga wakifurahia kwa pamoja baada ya kuibuka na ushidi wa bao 1-0 dhidi ya Ubembe FC kwenye mchezo wa fainali wa kuwania ng'ombe uliopigwa katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kilometa, Muheza juzi. Bao hilo pekee lilifungwa na Cosmas Kibo dakika ya 35. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Lule aanika tatizo Mbeya City

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, amefanya tathimini ya kikosi chake na kubaini kwamba wachezaji wake wameshuka kiwango kidogo hususan safu ya ushambuliaji kushindwa kutengeneza nafasi katika michezo minne iliyopita ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbeya City wanaingia kambini leo baada ya kumaliza mapumziko ya siku nne, tayari kwa maandalizi ya michezo yao ijayo ya Ligi Kuu Bara wakianza na Dodoma Jiji FC ugenini katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma Aprili 23, mwaka huu kabla tano baadaye kurejea jijini Mbeya kuikaribisha Biashara United.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema baada ya mapumziko mafupi sasa wanarejea kambini kesho (leo) na kuanza mazoezi kwa kufanyia kazi makosa hususan ni kuiweweka sawa safu yake ya ushambuliaji.

Alisema katika michezo minne ya mwisho waliyocheza ya ligi hawakufanya vizuri na safu yake ya ushambuliaji ilishindwa kutengeneza nafasi kama ilivyokuwa kwenye michezo iliyopita.

"Katika michezo iliyopita tulitengeneza nafasi nyingi sana na kushindwa kuzitumia, lakini michezo minne ya hivi karibuni karibuni tumeshindwa kutengeneza nafasi, hali hii ni hatari sana kwetu tunapaswa kuifanyia kazi haraka kipindi hiki cha mapumziko kwetu kabla ya mechi zijazo tuwe tumefanya kitu," alisema.

"Wakati tukifanyia kazi suala la washambuliaji, lakini pia kila nafasi hasa viungo na ulinzi ili kuhakikisha tunafikia malengo yetu ikiwamo kumaliza ligi tukiwa nafasi nne za juu kwenye msimamo," alisema Lule.

Alisema malengo yake makubwa ya kwanza ni kuhakikisha wanamaliza katika nafasi hizo nne za juu ili kuwa miongoni mwa timu nne zitakazokwenda kuwakilisha taifa katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Lazima tupambane kuhakikisha tunakusanya pointi katika michezo yetu ijayo tukianzia dhidi ya Dodoma Jiji FC, kwa sababu unaposhinda mechi moja unapanda juu na unapofungwa unashuka, hatutaki kushuka bali kupata matokeo mazuri na kufikia malengo yetu ya kumaliza nafasi nne za juu," alisema Lule.

Mbeya City iko nafasi ya tano ikiwa na pointi 25 chini ya Namungo FC ambao wako nafasi ya nne na alama zao 26 huku Azam FC wakishika namba ya tatu kwa kukusanya pointi 28 katika msimamo wa ligi hiyo.

## Nabi ampika Ngushi kuwa 9 ya Tanzania

**Na Saada Akida**

BAADA ya kumpa nafasi kwa mara ya kwanza tangu atokee katika chumba cha majeruhi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema bado anatakiwa kumjenga zaidi Crispin Ngushi ili aweze kuonyesha kiwango chake.

Ngushi juzi alipewa nafasi akitokea benchi katika mchezo dhidi ya Azam FC uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi na kumalizika kwa timu yao kuibuka na ushindi wa mabao 2-1, shukrani kwa Shabani Djuma na Fiston Mayele aliocheka na nyavu.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Nabi alisema Ngushi ni mchezaji mzuri na atakuwa msaada mkubwa kwa Tanzania hasa katika nafasi ya ushambuliaji, hivyomisimu miwili atahakikisha anamjenga na kumtengeneza kuwa bora.

Nabi alisema baada ya kurejea uwanjani akitokea kuuguza majeraha yake, anaendelea kumtengeneza awe imara zaidi na matarajio yake ni makubwa kwa nyota huyo kuja kuwa namba tisa bora kwa Tanzania.

"Ngushi ni mchezaji mzuri kuna vitu kidogo anatakiwa kupewa nina imani kwa miaka miwili ijayo, Tanzania itapata mshambuliaji (namba 9) mzuri ila kwa sasa naendelea kumtengeneza," alisema Nabi.

Alisema licha ya kuhakikisha anampika nyota huyo, anahitaji kuwa makini na kufuata kile anachompa katika mazoezi na kwenda kukionyesha uwanjani kama alivyofanya katika mechi dhidi ya Azam FC.

Matokeo hayo nanaifanya Yanga kuendelea kutesa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara wakiwa na alama 51 baada ya kushuka dimbani mara 19, msimu huu, huku wakiwa hawajapoteza mchezo hata mmoja wakiwa wameshinda mechi 16 na kutoka sare tatu.

## ZISIKUPITE

### DANJUMA ATAKIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL inamtaka winga wa Villarreal na Uholanzi, Arnaut Danjuma mwenye umri wa miaka 25, kuchukua nafasi ya mshambuliaji Sadio Mane, lakini Liverpool haina mpango huo kwa sasa hadi mwaka 2023. (***Goal***)

### HAG KUMSAJILI NEVES
KAMA kocha wa Ajax, Erik ten Hag akichaguliwa kuchukua nafasi pale Manchester United kama inavyotarajiwa, basi atamsajili kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25 kutoka Wolves. (***Sun***)

### WERNER KUTUA SERIE A
WAKALA wa mchezaji wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26, yupo nchini Italia akikutana na AC Milan, Juventus na Atalanta . (***Corriere dello Sport***)

### POGBA KURUDI JUVE
PAUL Pogba mwenye umri wa miaka 29, anapendelea kurudi Juventus kuliko kwenda Paris St-Germain baada ya muda wake kuisha majira ya joto. Lakini kwa upande wa Italia wana wasiwasi kuhusu fedha anazotaka kulinganisha na umri wake. (***Tuttosport***)

### DEPAY ATAKIWA EPL
ARSENAL, Everton na Newcastle wote wameonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay kutoka Barcelona. (***Superdeporte***)

### GAKPO AITAKA ARSENAL
WINGA wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 22, ameweka wazi mapenzi yake kwa Arsenal huku akiendelea kuunganishwa na wenyeji wa klabu nyingine ikiwamo Manchester United na Liverpool. (***Goal***)

### LUKAKU ATAKIWA MILAN
VIONGOZI wa ngazi za juu Inter Milan sasa wanamtaka mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28 arudi klabuni hapo. (***Mirror***)

### JUSTE AWANIWA LEICESTER
KLABU ya Leicester City imeonyesha nia ya kumtaka mlinzi wa FC Mainz, Jeremiah St. Juste mwenye umri wa miaka 25. (***Bild - via Leicester Mercury***)

### NEWCASTLE KUMKOSA SANCHEZ
KLABU ya Brighton hawana mpango wa kumuuza kipa wake Sanchez mbali ya kuwa Newcastle wameonyesha nia ya kumhitaji kipa huyo Mhispania mwenye umri wa miaka 24. (***Football Insider***)

### LEWANDOWSKI ANUKIA BARCA
BARCELONA ina imani kuwa ina nafasi kubwa ya kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, msimu huu wa majira ya joto. (***Sport***)

### BAYERN, GRAVENBERCH SAFI
KIUNGO wa kati wa Ajax na Uholanzi, Ryan Gravenberch mwenye umri wa miaka 19, amekubali kuingia mkataba binafsi na Bayern Munich. (***Bild - via Bundesliga***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA APIGIWA SALUTI NA WACHEZAJI MADRID

**Ili kufika mbali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya unahitaji mchezaji kama yeye, ambaye...**

**LONDON,** ENGLAND

KARIM Benzema anacheza "msimu wa maisha yake" huku wachezaji wenzake wa Real Madrid wakimsifu nahodha huyo baada ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea, Jumatano.

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa, Benzema alifunga mabao yote matatu ya timu yake katika ushindi wao wa 3-1 dhidi ya Chelsea Jumatano, kwenye mechi ya kwanza ya robo fainali.

Kiwango hicho jijini London kilimfanya Benzema afikishe mabao 37 na kutoa asisti 13 katika mechi 36 msimu huu.

Ushiriki wake wa mabao 50 jumla, unamuweka juu ya wachezaji wote kutoka ligi tano kuu za Ulaya, huku Robert Lewandowski wa Bayern Munich akiwa wa pili kwenye orodha hiyo akiwa amehusika mara 49 (mabao 45, asisti nne).

Mabao kumi kati ya hayo kutoka kwa Benzema yamepatikana katika michezo yake minne iliyopita, akiwa na hat-trick ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain na Chelsea na akifunga mabao mawili ya LaLiga dhidi ya Real Mallorca na Celta Vigo.

**Alipokosekana dhidi ya Barcelona kutokana na jeraha, Madrid walionekana kupotea na wakachapwa mabao 4-0 kwenye El Clasico.**

Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel alitoa sauti ya kukata tamaa baada ya mchezo huo, akionya juu ya hatari ya timu yake kuangamizwa katika mechi ya pili wiki ijayo ikiwa watatoa matokeo mengine yasiyofaa.

Lakini Madrid walifurahishwa na matokeo hayo, huku mlinzi nyota David Alaba akizungumzia zamu ya kushinda mechi ya Benzema mwenye umri wa miaka 34.

"Anachofanya msimu huu ni cha ajabu," alisema Alaba baada ya mechi.

"Naona jinsi anavyofanya kazi kwa bidii, na ana msimu wa maisha yake, ana umakini mkubwa na ana njaa ya kufunga mabao. Anajipanga vema kwa kila mchezo, haswa mechi kama hizi za usiku wa leo (juzi). Nina furaha kuwa naye kama mchezaji bora. mshiriki wa timu."


Kipa Thibaut Courtois alizungumzia "matokeo muhimu" ya Madrid na kubainisha shujaa wa hat-trick, akisema: "Ili kufika mbali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya unahitaji mchezaji kama Benzema."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,119

MECHI KALI
STUTTGART
VERSUS
BORUSSIA DORTMUND
1 | 3.65
X | 3.85
2 | 1.86

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# NAGELSMANN: KIPIGO CHA BAYERN UEFA SAHIHI KABISA

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, amekiri kuwa timu yake ilistahili kupoteza mechi yao ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Villarreal, Jumatano.

Arnaut Danjuma alifunga bao pekee la ushindi katika dakika ya nane, na umaliziaji wa ovyo ndio uliowazuia wenyeji kupata bao la kuongoza.

Matokeo hayo yamekuwa mara ya kwanza kwa Bayern kushindwa kufunga katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu Februari 2019, na hivyo kuhitimisha mfululizo wa mechi 30 ambapo walikuwa wamefunga angalau mara moja.


Ingawa Nagelsmann alikubali kuwa Villarreal walikuwa wanastahili ushindi, bado anaamini kuwa timu yake ina kile kinachohitajika kugeuza mechi hiyo.

"Tulistahili kupoteza. Hatukuwa wazuri leo (juzi). Katika kipindi cha kwanza, tulikosa nguvu katika ulinzi na tulipata nafasi chache sana," alisema Nagelsmann akiiambia DAZN.

"Kipindi cha pili ulikuwa mchezo wa kipumbavu kabisa. Tuliachana na mchezo kwa sababu tulikuwa na hamu ya kutaka kufunga.

"Nadhani wangeweza kufunga mabao machache zaidi dhidi yetu, lakini ilikuwa 1-0. Hatujacheza mchezo mzuri leo(juzi) katika nyanja zote.

"Lakini ni 1-0 tu na tunapaswa kuonyesha upande mwingine wetu katika mkondo wa pili; tunajua jinsi ya kufanya hivyo na nadhani tutafanya."



## Eriksson aipa England nafasi

**LONDON,** England

ENGLAND inaweza kuchukuliwa kama "inayopewa nafasi kubwa zaidi" kwenye Kombe la Dunia la 2022, kwa mujibu wa kocha wa zamani wa timu hiyo, Sven-Goran Eriksson.

Kikosi cha Gareth Southgate kilitinga nusu fainali Urusi mwaka 2018, ikilingana na juhudi bora zaidi za England kwenye Kombe la Dunia tangu washinde katika ardhi ya nyumbani mwaka 1966.

England ndipo ilipocheza fainali ya michuano hiyo mikubwa kwa mara ya kwanza tangu 1966 ilipomenyana na Italia kwenye michuano ya Euro 2020 mwaka jana, na kupoteza kwa mikwaju ya penalti.

Eriksson aliiongoza England katika Fainali za Kombe la Dunia za 2002 na 2006, na kufika robo-fainali ya kila mchuano, huku pia akifika hatua ya nane bora kwenye Euro 2004.

Eriksson aliiambia Stats Perform: "Nadhani ni moja ya timu kubwa ambazo zinaweza kushinda, na labda ndizo zinazopendwa zaidi.

"Sina hakika jinsi Brazil na Argentina zilivyo na nguvu kwa wakati huu, lakini Ulaya, Italia (hawapo). Hispania, sidhani kama wanatosha kushinda pia. Ujerumani, huwezi kujua wanaweza kushinda. Ubelgiji ni timu nzuri kila wakati."




,012,860

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/04/22 | 17:00 | Watford vs Leeds | 2.75 | 3.29 | 2.49 |
| 02. 09/04/22 | 17:00 | Preston vs QPR | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 09/04/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.63 | 3.13 | 2.63 |
| 04. 09/04/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Union Berlin | 2.69 | 3.19 | 2.59 |
| 05. 09/04/22 | 20:00 | Amiens vs Bastia | 2.63 | 2.93 | 2.78 |
| 06. 10/04/22 | 15:15 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.37 | 3.48 | 2.73 |
| 07. 10/04/22 | 16:00 | Sivasspor vs Basaksehir | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 10/04/22 | 16:00 | Brentford vs West Ham | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 10/04/22 | 16:00 | Norwich City vs Burnley | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 10. 10/04/22 | 16:00 | Brest vs Nantes | 2.43 | 3.22 | 2.92 |
| 11. 10/04/22 | 17:15 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.78 | 3.13 | 2.63 |
| 12. 10/04/22 | 17:30 | St. Gallen vs FC Basel | 2.39 | 3.53 | 2.68 |
| 13. 10/04/22 | 20:00 | Strasbourg vs Lyon | 2.60 | 3.30 | 2.65 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 08/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 3986 | Beitar Tel Aviv Ramla vs Hapoel Acre | 2.71 | 3.16 | 2.61 |
| 17:00 | 1708 | Botev Vratsa vs Slavia Sofia | 3.41 | 3.22 | 2.02 |
| 17:00 | 3849 | Ararat Armenia vs Urartu | 1.64 | 3.40 | 5.06 |
| 17:30 | 5016 | Taborsko vs Opava | 2.13 | 3.22 | 3.12 |
| 18:00 | 1158 | Lahti vs VPS Vaasa | 2.26 | 3.07 | 3.02 |
| 18:00 | 3570 | Seinajoen JK vs HJK Helsinki | 3.74 | 3.06 | 1.97 |
| 19:00 | 1533 | FC KoÅiice vs FK Puchov | 1.44 | 4.38 | 5.64 |
| 19:00 | 3043 | Resovia Rzeszow vs Podbeskidzie Bie | 3.21 | 3.16 | 2.12 |
| 19:00 | 4974 | Zaglebie Lubin vs Stal Mielec | 1.90 | 3.31 | 3.70 |
| 19:30 | 3365 | FC Liefering vs Wacker Innsbruck | 2.11 | 3.45 | 2.97 |
| 19:30 | 3922 | Blau Weiss Linz vs Amstetten | 1.79 | 3.51 | 3.90 |
| 19:30 | 5029 | Liebherr Gak vs Rapid Vienna II | 2.16 | 3.35 | 2.96 |
| 19:30 | 5607 | Austria Vienna II vs FC Juniors OO | 1.77 | 3.61 | 3.90 |
| 20:00 | 1267 | Chateauroux vs Red Star | 2.09 | 3.20 | 3.40 |
| 20:00 | 2424 | Saint Brieuc vs Laval | 2.70 | 2.90 | 2.70 |
| 20:00 | 3209 | Sete 34 FC vs Chambly | 2.52 | 3.01 | 2.81 |
| 20:00 | 3818 | Penafiel vs Varzim | 2.02 | 3.24 | 3.54 |
| 20:00 | 4366 | Creteil vs Orleans | 2.57 | 3.06 | 2.71 |
| 20:00 | 5191 | Buchbach vs Memmingen | 2.12 | 3.45 | 2.96 |
| 20:00 | 5395 | Avranches vs Villefranche Sur Saone | 3.15 | 3.15 | 2.22 |
| 20:30 | 5837 | Gaziantep BB vs Trabzonspor | 3.29 | 3.34 | 2.12 |
| 20:30 | 5854 | Neuchatel Xamax vs FC Thun | 2.58 | 3.41 | 2.39 |
| 21:00 | 1142 | GO Ahead Eagles vs Willem II Tilburg | 2.11 | 3.18 | 3.42 |
| 21:00 | 1304 | FC Volendam vs De Graafschap | 2.51 | 3.39 | 2.56 |
| 21:00 | 1879 | SBV Excelsior vs Telstar | 1.56 | 4.24 | 4.83 |
| 21:00 | 2191 | FC Eindhoven vs Almere City | 2.06 | 3.49 | 3.20 |
| 21:00 | 2248 | FC Oss vs Jong PSV | 2.43 | 3.54 | 2.56 |
| 21:00 | 2471 | ADO Den Haag vs Helmond Sport | 1.42 | 4.73 | 5.91 |
| 21:00 | 2606 | Den Bosch vs Dordrecht | 1.86 | 3.75 | 3.55 |
| 21:00 | 3049 | Excelsior Virton vs Lommel United | 3.65 | 3.69 | 1.85 |
| 21:00 | 4338 | Zalaegerszegi TE vs Budapest Honved | 2.41 | 3.30 | 2.62 |
| 21:00 | 4580 | Roda Kerkrade vs Jong Ajax | 1.99 | 3.70 | 3.21 |
| 21:00 | 4867 | Emmen vs Jong AZ Alkmaar | 1.37 | 4.74 | 6.91 |
| 21:00 | 5106 | NAC Breda vs VVV Venlo | 1.99 | 3.59 | 3.30 |
| 21:00 | 5747 | Maastricht vs Jong Utrecht | 2.81 | 3.50 | 2.26 |
| 21:30 | 2324 | LKS Lodz Pss vs Sandecja | 1.91 | 3.30 | 3.64 |
| 21:30 | 2907 | Stuttgart vs Borussia Dortmund | 3.65 | 3.85 | 1.86 |
| 21:30 | 5110 | Pogon Szczecin vs Wisla Plock | 1.46 | 3.90 | 6.24 |
| 21:45 | 1383 | Shelbourne vs Shamrock Rovers | 5.45 | 3.60 | 1.57 |
| 21:45 | 1946 | Bray Wanderers vs Treaty United | 2.01 | 3.25 | 3.40 |
| 21:45 | 4254 | Drogheda Utd vs Bohemians FC | 4.28 | 3.35 | 1.76 |
| 21:45 | 5350 | Queen of South vs Partick Thisle | 3.06 | 3.25 | 2.22 |
| 21:45 | 5419 | Cobh Ramblers vs Waterford Utd | 5.43 | 4.07 | 1.49 |
| 21:45 | 5855 | St Patricks vs Dundalk FC | 1.95 | 3.20 | 3.64 |
| 22:00 | 1834 | Lorient vs St Etienne | 2.38 | 3.13 | 3.08 |
| 22:00 | 2559 | UD Logrones vs Tudelano | 1.48 | 3.55 | 7.01 |
| 22:00 | 3703 | Newcastle vs Wolverhampton | 2.22 | 3.10 | 3.35 |
| 22:00 | 3781 | Sevilla FC vs Granada | 1.42 | 4.34 | 7.87 |
| 22:00 | 4395 | Lugo vs FC Cartagena | 2.45 | 3.21 | 2.77 |
| 22:15 | 2568 | Gil Vicente vs Moreirense | 1.75 | 3.58 | 4.47 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# SURE BOY AANIKA CHANGAMOTO KUICHEZEA YANGA CHAMAZI

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Yanga, Salum Abubabakar 'Sure Boy' ameeleza furaha yake kurejea tena kwenye uwanja aliouzoea wa Azam Complex, Chamazi akiwa na timu yake mpya, huku akipata ushindi wa mabao 2-1.

**Akizungumza mara baada ya mechi ya Ligi Kuu kati ya timu yake mpya ya Yanga na waajiri wake wa zamani, Azam FC, Sure Boy alisema ilikuwa ni mechi yenye hisia, kwani alikuwa akicheza dhidi ya timu iliyomlea, na timu yake mpya, pia kwenye uwanja ambao wameuzoea sana, ndiyo maana hata kiwango chake kilikuwa ni kikubwa.**

"Tumepata pointi tatu, mechi ilikuwa ngumu, timu zote tulicheza vizuri, pale kati tulikuwa na kazi kwa sababu wote tulikuwa tunafahamiana, mimi nimecheza kwenye timu ya Azam na wachezaji waliokuwa wanacheza nafasi ya kiungo, kwa hiyo kila mmoja alikuwa anaonyesha nini anacho mguuni, si kweli kama tulikuwa tumekamiana sana kama baadhi ya watu wanavyosema. Wao wameuzoea uwanja na mimi pia nimeuzoea pia na tumezoeana hata mazoezi tulikuwa tunacheza wote, kwa hiyo ilikuwa ni kazi kubwa pale katikati, naamini tulicheza vizuri wote, mimi nilitaka kuonyesha vitu na wao hawakuniacha, ila hatukukamiana," alisema.



Sure Boy alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo la msimu huu, akitokea Azam, na haikuwa mara ya kwanza Yanga kufanya jaribio la kutaka kumsajili mchezaji huyo, ambaye mara kwa mara lilikuwa linagonga mwamba.

Mchezaji huyo anayecheza nafasi ya kiungo, ni mtoto wa winga wa zamani wa Yanga, Aboubakar Salum, aliyetamba na timu hiyo akitokea Sigara, miaka ya katikati ya 1980 na kupewa jina la 'Sure Boy' ambalo mtoto wake kwa sasa analitumia.



# Kidunda ajifua kurudiana na Katompa

**Na Saada Akida**

BONDIA Mtanzania Seleman Kidunda, amesema atatumia miezi mitatu vizuri kujiandaa na pambano lake dhidi ya Tshimanga Katompa kutoka Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC).

Pambano hilo la marudiano linalotarajiwa kupigwa Julai mwaka huu mkoani Songea, limekuja baada ya lile la awali kushindwa kumalizika kutokana na Kidunda kupasuka paji la uso.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kidunda alisema ana miezi mitatu ya kujiandaa na pambano hilo na kuhakikisha anatumia vizuri muda huo kujiandaa kikamilifu kurudiana na Katompa.

Alisema pambano lililopita lilihairishwa kwa sababu ya kupata jeraha jambo ambalo kanuni na sheria ya mchezo huo hairuhusu mpambano kuendelea, hivyo sasa anajipanga vizuri kukabiliana na mpinzani wake huyo.

"Niko fiti kurudiana na Katompa, muandaaji aweke pambano ili niingie mzigoni kuwapa raha Watanzania na mashabiki wa ngumi, lakini pia kuhakikisha tunaliheshimisha taifa katika mchezo huu," alisema Kidunda.

Alisema anaendelea na mazoezi na ameanza muda mrefu kujiimarisha zaidi kwa kujiandaa na pambano hilo ambalo hatakubali hali ya kupasuka kujirudia tena.

Naye muandaaji wa pambano hilo, Selemani Semunyu, amewaomba mashabiki wa ngumi nchini kujiandaa kwa ajili ya kumsapoti bondia huyo katika pambano hilo.

"Kidunda na Katompa watarudiana tena baada ya pambano la kwanza kuahirishwa kwa matokeo ya sare, hili pambano la Julai ndio litakalotoa mbabe wa ngumi kati ya mabondia hao wawili," alisema Semunyu.

# Michezo

Ijumaa Aprili 8, 2022

Nipashe




Benzema apigiwa saluti Madrid UKURASA 21

TWENDE SASA...



Winga wa Simba, Bernard Morrison (katikati), akishangilia kwa staili ya kuserebuka sambamba na Clatous Chama (kushoto) na Chris Mugalu, baada ya kuifungia timu yake bao la kwanza wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Yanga: Bado wao

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya kuichapa Azam mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Kocha Mkuu wa Yanga Nasreddine Nabi, amesema "tulistahili kupata ushindi" kwa sababu ya kuzitumia vizuri nafasi walizozipata, huku Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli akisema wamepangua mechi mbili ambazo wapinzani wao, Simba walidai wataepoteza, kwa hiyo sasa imebaki zamu yao kufungwa.

Yanga ilipata ushindi huo shukrani kwa Fiston Mayele na Shabani Djuma aliyefunga kwa mkwaju wa penalti, hivyo kuifanya timu yao kuendelea kujikita kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kufikisha pointi 51.

Nabi aliwapongeza wachezaji wake kwa kujituma kwa sababu mechi ilikuwa ngumu, hasa kipindi cha kwanza kwani kila mchezaji alicheza bila kufuata maelekezo ya nafasi ambayo alipewa kuifanyia kazi.

"Hawakucheza kwenye nafasi, ndiyo maana tuliwapa uwanja mkubwa wapinzani kutawala, lakini kipindi cha pili tulijirekebisha, walicheza kwenye nafasi na kufuata maelekezo, tukaishika mechi na kutumia nafasi chache zilizopatikana kupata ushindi," alisema Nabi raia wa Tunisia.

Kwa upande wa Bumbuli alisema: "Azam walicheza vizuri sana, sisi tulikuwa bora kwenye utumiaji nafasi, kwa ushindi huu unatupa nafasi nzuri ya kujiamini kwenda kwenye mechi yetu ya terehe 30 na hao ambao walisema kuwa wanatupa mechi nne za kupoteza, mbili tayari tumeshazipangua, bado wao sasa tarehe 30, halafu katika hizo mechi nne itabaki moja, wacha waendelee kupiga mahesabu ya vidole," alisema Bumbuli.

Naye Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, alisema mchezo ulikuwa mgumu timu zote zilicheza vizuri kipindi cha kwanza, lakini cha pili hawakuweza kufanya vizuri.

"Mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa, tulifanya makosa Yanga wakatuadhibu na sasa tunasahau matokeo ya mechi hii tunarudi uwanjani kurekebisha makosa yetu na tukijiandaa na mchezo ujao wa Kombe la FA," alisema Moallin.

# Simba yafanya yake Mkwakwani

## Kagere aipa ushindi jua likizama, huku Morrison akizidi kung'ara, waifuta Polisi Tanzania...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya pili ya nyongeza, lililowekwa wavuni na Mnyarwanda Meddie Kagere, liliiwezesha Simba kuondoka kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wenyeji, Coastal Union, ikiwa ni mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Lilikuwa ni bao lililosubiriwa kwa hamu na wanachama na mashabiki wa timu hiyo, kwani baadhi walikuwa wameshakata tamaa wakidhani mechi hiyo itaisha kwa sare ya bao 1-1.**

Mpira mrefu uliopigwa, ulitua kwenye msitu wa wachezaji wa timu zote mbili, lakini ulidunda wakati mchezaji mmoja wa Coastal akiwa karibu kuuokoa, Kagere ambaye aliingia kipindi cha pili alikuwa makini kuufuatilia na kuukwamisha wavuni, akizima ndoto za wenyeji kupata angalau sare kwenye mechi hiyo.

Hilo linakuwa ni bao la sita kwa Kagere kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Ni mechi ambayo angalau ilichangamka mara baada ya Coastal Union kurudisha bao dakika ya 76, lililofungwa na kiungo mkabaji raia wa Nigeria, Victor Akpan kutokana na makosa ya wachezaji wa Simba kutokwenda kumkaba akiwa peke yake, akapiga 'shuti mchinjo' lililoonekana kama linatoka nje, lakini mpira ukajaa wavuni.

Mfungaji alipasiwa mpira wa kona, huku wachezaji wa Simba wakiwa wamesimama golini bila kwenda kumkaba.

Kona hiyo ilipatikana, baada ya Aishi Manula kuokoa shambulizi la hatari lililofanywa na Vicent Aboubakar ambaye alipiga mpira ulioonekana unakwenda wavuni, lakini kipa huyo alipaa juu na kuupiga ngumi mpira uliotoka kona iliyozaa bao.

Kabla ya bao hilo, Simba ilikuwa imetangulia kwa bao la Mghana Bernard Morrison dakika ya 39 lililotokana na makosa ya wachezaji wa Coastal Union na kipa wao.

Kujiamini kuanzia mpira nyuma kuli- rison na kuujaza wavuni kirahisi dakika ya 39.

Alikuwa ni kipa Mbissa alipomuanzia Jacson Shiga, aliyeupeleka kwa Miraji Wandi ambaye aliupiga mpira ulionasa kwenye mguu wa mfungaji, kabla ya kuukwamisha wavuni

Mechi ilianza kwa kupooza, wachezaji wa pande zote mbili wakipasiana pasi fupi fupi, ambazo mara nyingi zilikuwa zikikwama kwa wapinzani wao.

Iliwachukua dakika 12 kwa shuti la kwanza kupigwa, na walikuwa ni Coastal Union kupitia kwa Haji Ugando, ambaye aliupata mpira akiwa upande wa kushoto mwa uwanja, akachia shuti lililotoka kidogo nje ya lango la Simba.

Ikawa kama imeamshwa usingizini kwani walijibu dakika tatu baadaye, baada ya Bernard Morrison kuupata mpira akiwa ndani ya eneo la hatari, akaupiga mpira kwa kuukata, ukatoka nje kidogo, baada ya kumbabatiza kipa Mussa Mbissa.

Hata kabla ya kufunga bao la pili, Simba

Morrison, Chris Mugalu na Yusuph Mhilu aliyeingia kipindi cha pili.

Kwa ushindi huo, Simba imefikisha pointi 40, ikicheza mechi 18, ikizidiwa pointi 11 na vinara Yanga ambayo imefikisha pointi 51 zilizotokana na michezo 19, huku Coastal ikiwa kwenye nafasi ya 12, ikisalia na pointi zake 21.

Simba sasa itaifuata Polisi Tanzania katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Jumapili wiki hii kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi na baada ya hapo itarejea Dar es Salaam kuisubiri Orlando Pirates ya Afrika Kusini tayari kwa mchezo wao wa kwanza wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Aprili 17, mwaka huu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >